

**MCHANGO WA SITIARI NA METONIMU KATIKA UZUAJI WA
POLISEMIA KATIKA KISWAHILI**

**(THE ROLE OF METAPHORS AND METONYMS IN THE
FORMATION OF POLYSEMY IN KISWAHILI)**

MARK ELPHAS MASIKA

C50/28186/2019

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU
CHA KENYATTA**

APRIL, 2024

IKIRARI

Tasufu hii ni kazi yangu asilia na haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

Sahihi... 

Tarehe 24/04/2024

Mark Elphas Masika

C50/28186/2019

Tasufu hili imewasilishwa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyechaguliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi... 

Tarehe 24/04/2024

Dkt. Leonard Mwita Chacha

Idara ya Kiswahili

Shule ya Sheria, Fani na Sayansi ya Jamii

Chuo Kikuu cha Kenyatta

TABARUKU

Utafiti huu nautabaruku kwa wavyele wangu wapendwa, Martin Masika
Mwelesie na Jane Moragwa. Mola awatunuku baraka. Nisingefaulu bila
mchango wenu.

SHUKRANI

Namshukuru Mola kwa kunipa uwezo, neema na hekima ya namna ya kufanya utafiti huu tangu mwanzo hadi nikaumaliza. Shukrani za dhati kwa msimamizi wangu Dkt. Leonard Chacha Mwita kwa kunielekeza, kunikosa kunishauri na kunitia moyo wakati wa kufanya uchunguzi huu. Mola akupe maisha marefu yenye mafanikio na baraka tele.

Pia nawashukuru wahadhiri wote walionifunza na kunikuza kitaaluma: Dkt. Ngugi Boniface, Dkt. Osore Miriam. Mw. Mudhune Everline, Prof. Kitula King'ei, Prof. Ileri Mbaabu, Dkt Masinde Edwin na Dkt. Ngugi Pamela. Mola awabariki. Aidha, shukrani ziwaendee wanafunzi wenzagu wa uzamili: Priscah, Nelly, Catherine, Devica, Joyce, Evans na Mofart walionihimiza kila mara nisikate tamaa. Kwenu nyote nawatolea shukrani za pekee kwa kunipa nafasi ya kushirikiana nanyi wakati nilihitaji msaada wenu. Kwenu nyote, Mola awabariki.

Kadhalika, nawashukuru wavyele wangu; Martin Mwelesie Masika na Jane Moragwa Masika kwa kuniombea na kunitia moyo katika safari hii ya uchunguzi. Mola awape maisha mema yenye neema na baraka tele. Mwisho, Shukrani zangu za dhati pia ziwaendee akraba zangu, Juma, David, Joyce, Ruth na Meshack kwa kuniombea na kunitia moyo kila wakati. Mola awabariki na awazidishie maisha yenye baraka.

YALIYOMO

IKIRARI	Error! Bookmark not defined.
TABARUKU	iii
SHUKRANI	iv
YALIYOMO	v
MAJEDWALI	viii
MICHORO	ix
UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU	x
ORODHA YA VIFUPISHO	xi
IKISIRI	xii
ABSTRACT	xiii
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.0 Usuli wa mada.....	1
1.1 Suala la utafiti	4
1.2 Malengo ya utafiti	4
1.3 Maswali ya utafiti	5
1.4 Sababu za kuchagua mada	5
1.5 Upeo na mipaka ya utafiti	6
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada.....	6
1.6.1 Yaliyoandikwa kuhusu polisemia	7
1.6.2 Yaliyoandika kuhusu sitiari.....	8
1.6.3 Yaliyoandikwa kuhusu metonimu.....	9
1.7 Misingi ya nadharia.....	10
1.7.1 Nadharia ya semantiki tambuzi	11
1.7.2 Mihimili ya nadharia ya semantiki tambuzi.....	12
1.8 Mbinu za utafiti.....	14

1.8.1 Muundo wa utafiti	14
1.8.2 Eneo la utafiti	14
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli	14
1.8.4 Mbinu za ukusanyaji data.....	15
1.8.5 Uchanganuzi wa data	16
1.8.6 Uwasilishaji wa matokeo	16
1.8.7 Maadili ya utafiti	16
1.9 Hitimisho.....	17
SURA YA PILI: POLISEMI AMBAZO ZIMEUNDWA KUTOKANA NA SITIARI NA METONIMU	18
2.0 Utangulizi.....	18
2.1 Polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari katika Kiswahili.....	19
2.2 Polisemi ambazo zimeundwa kutokana na metonimu katika Kiswahili...37	
2.3 Hitimisho.....	43
SURA YA TATU: UAINISHAJI WA POLISEMI.....	45
3.0 Utangulizi.....	45
3.1 Uainishaji wa polisemi za Kiswahili.....	46
3.2 Uainishaji wa polisemi kiutambuzi.....	46
3.3 Uainishaji wa polisemi kwa mtazamo wa kitabia.....	48
3.3.1 Polisemi za wanyama	48
3.3.2 Polisemi za wadudu.....	51
3.3.3 Polisemi za ndege.....	51
3.4 Uainishaji wa kiuamilifu.....	52
3.4.1 Polisemi zinazorejelea utendakazi wa kitu.....	52
3.4.2 Polisemi za chombojikoni	53
3.5 Uainishaji wa Kijiografia.....	54

3.6. Uainishaji wa polisemi kihusiano	54
3.6.1 Polisemi zenye uhusiano wa ki-mahali	55
3.6.2 Polisemi zenye uhusiano wa sifa.....	56
3.6.3 Polisemi zenye uhusiano wa Kiumbo	58
3.7 Hitimisho.....	60
SURA YA NNE: MCHAKATO AMBAO SITIARI NA METONIMU	
HUPITIA KUUNDA POLISEMI.....	62
4.0 Utangulizi.....	62
4.1 Mchakato ambao sitiari hupitia kuunda Polisemi	62
4.2 Mchakato ambao metonimu hupitia kuunda polisemi	70
4.3 Hitimisho.....	73
SURA YA TANO: MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO	
YA UTAFITI.....	74
5.0 Utangulizi.....	74
5.1 Muhtasari wa tasnifu	74
5.2 Matokeo ya utafiti	76
5.3 Mapendekezo ya utafiti.....	78
5.4 Hitimisho.....	79
MAREJELEO	80
VIAMBATISHO	83
Kiambatisho A: Kibali cha kukubalika kwa pendekezo	83
Kiambatisho B: Kibali cha idhini ya kutekeleza Utafiti	84
Kiambatisho C: Kibali cha NACOSTI	85

MAJEDWALI

Jedwali 3.1: Polisemi zenye uhusiano wa ki-mahali	55
Jedwali 3.2: Polisemi zenye uhusiano wa sifa.....	57
Jedwali 3.3: Polisemi zenye uhusiano wa kiumbo	59

MICHORO

Mchoro 4.1: Maumbo ya kidhahania.....	64
Mchoro 4.2: Kufananisha	65
Mchoro 4.3: Matumizi ya leksimu	67
Mchoro 4.4: Leksimu ambazo zina maana zaidi ya mbili	68
Mchoro 4.5: Metonimu	72

UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU

- Fahiwa: Dhana ya kiisimu inayowakilisha neno, tofauti na kitajwa chenyewe.
- Leksia: Kipashio kidogo zaidi katika lugha chenye kujisimamia kama neno kamili.
- Metonimu: Neno au jina linalotumiwa kurejelea kitu kingine ambacho kinahusiana nacho kwa namna fulani.
- Polisemia: Ni utaratibu wa neno moja kuweza kuwakilisha zaidi ya dhana moja.
- Sitiari dhanifu: Ni sitiari au ulinganifu wa kitamathali ambapo kitu au dhana moja hueleweka kwa misingi ya dhana/ kitu kingine.
- Sitiari: Ni mchakato ambapo dhana moja inaelezwa kupitia dhana nyingine tofauti.

ORODHA YA VIFUPISHO

K.M:	Kwa mfano
K.V:	Kama vile
KKS:	Kamusi ya Kiswahili Sanifu

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuangazia mchango wa sitiari na metonimu katika uzuaji wa polisemia katika Kiswahili ambapo uliweza kupambanua namna metonimu na sitiari zinavyoweza kuzua maana mpya ya maneno ya Kiswahili. Pia ulitusaidia kufahamu athari ya metonimu na sitiari katika uzuaji wa polisemia katika Kiswahili. Kimsingi polisemi ni leksimu moja yenye maana nyingi ambazo zinahusiana kwa njia moja au nyingine (Chacha na Pendo, 2019). Pia kuna njia zingine za uzuaji wa polisemi kwa mfano ukopaji, mabadiliko katika matumizi ya neno, na ufasiri mpya wa homonimu. Kuna baadhi ya wataalamu ambao wamezungumzia polisemia kama vile Mwendamseke (2016) aliyehandika makala kuhusu uelekeo wa maana za kipolisemia katika msamiati wa Kiswahili. Naye Gaichu (2013) alishughulikia uchunguzi wa sitiari dhanifu katika methali za Kiswahili. Utafiti huu wa sitiari na metonimu ndio usiodhihirika moja kwa moja. Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo: Kubainisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu katika Kiswahili, kuainisha polisemi katika lugha ya Kiswahili, kudhihirisha mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia kuunda polisemi katika Kiswahili. Nadharia ya semantiki tambuzi iliongoza utafiti huu. Nadharia hii ni sehemu ya nadharia ya Isimu Tambuzi ambayo ina misingi katika saikolojia tambuzi (Vyvyan & Greens, 2006). Data husika ilikusanywa maktabani. Maktabani, maneno ambayo ni polisemi na yameundwa kwa sitiari na metonimu kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)* yalikusanywa. Mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi ilitumika katika uteuzi wa sampuli. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo na majedwali ili iweze kueleweka. Kutokana na data ya utafiti huu, imebainika kuwa kuna baadhi ya polisemi zilizojitokeza ndani ya homonimu. Kwa mfano, tata² na chuo¹. Pia, imebainika kuwa data hiyo ilikuwa na polisemi za majina ya wanyama, wadudu na ndege. Hata hivyo, imebainika kuwa sitiari huwa na maeneo mawili ya ufahamu: moja ni ile inayotokana na maumbo tunayoyaona na nyingine ni ile ya kidhahania. Hiyo ya kwanza inaitwa eneo chasili na ya pili eneo lengwa. Kwa mfano, sitiari “Maria ni chui” maumbo tunayoyaona (eneo chasili) ni Maria na chui na maumbo ya kidhahania (eneo lengwa) ni ukali. Kwa upande mwingine, imebainika kuwa metonimu huwa na eneo moja. Kwa mfano, leksimu *kiti* eneo lake ni uongozi. Tafiti zingine zinaweza kufanywa kuhusu mchango wa mbinu zingine za lugha kama vile tashibihi, lakabu na jazanda yaani; namna ambavyo mbinu hizo zinaweza kuchangia pia katika kuunda polisemia katika Kiswahili.

ABSTRACT

This research intended to explore the role of metaphors and metonyms in the formation of polysemy in Kiswahili where the researcher was able to identify how metonyms and metaphors can spark new meanings in Kiswahili words. It helped us to understand the effect of metaphors and metonyms, in the formation of polysemes in Kiswahili. Apart from metaphors and metonyms there are also other ways of forming polysemes in Kiswahili for example word borrowing, changes in word usage and new interpretation of homonyms. There are some scholars who have done research on polysemy such as Mwendamseke (2017), who wrote an article on polysemous meanings in Kiswahili vocabulary. Gaichu (2013) also carried out research of conceptual metaphors in Kiswahili proverbs. However, in their reasearches, the aspect of metaphor and metonym does not manifest itself directly and this research aims at achieving that. This research will be guided by the cognitive semantic theory. This theory is part of cognitive linguistics theory rooted in cognitive psychology (Vyvyan & Greens, 2006). This theory helped in achieving the research objectives. These objectives are: identify polysemes that are formed from metaphors and metonyms in Kiswahili, to categorize different forms of polysemes in Kiswahili language, to illustrate the process in which metaphors and metonyms go through in order to form polysemes in Kiswahili, relevant data was collected in the library. In the library, the researcher collected words that are polysemes and are formed by metaphors and metonyms from *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2018). Deliberate sampling technique was used in sample selection. Data was analyzed and presented using descriptions, tables and drawings so that it can be understood. From the data of this research, it has been found that there are some polysemes that emerged within homonyms. For example, complexity² and college¹. This research has identified that the data contained polysemous names of animals, insects and birds. However, it has been found that metaphors have two areas of understanding: one is source domain and the other one is target domain. For example, the metaphor "Maria is a leopard" the source domain is Maria and the leopard on other hand, the target domain is severity. On the other hand, it has been noted that metonyms tend to have one area of understanding. For example, the lexicon 'seat' stands for leadership. Other studies can be done on the role of other stylistic devices of language such as similes, nick names and images, and how these stylistic devices of language can also contribute to the formation of polysemy in Kiswahili

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa mada

Lugha kama kifaa cha kupashana habari baina ya binadamu hutumia sauti nasibu na ishara zilizoteuliwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za wanajamii wanaohusika. Rajab (2017) akimnukuu Halliday (1964) anadai kuwa lugha inakua kupitia tajriba za kijamii wala si katika ombwe tupu, na hapo ndipo inapata msingi, sura na ruwaza zake. Uamilifu wa lugha kama tukio la kijamii, ni matumizi yake kama tukio la mawasiliano baina ya wanajamii.

Mada ya utafiti huu inapatikana katika eneo jumla la isimu maana. Kwa mujibu wa *Kamusi Sanifu ya Isimu na Falsafa ya Lugha (2004)*, semantiki ni taalumu ya isimu inayojishughulisha na uchanganuzi na uchambuzi wa maana za maneno au tungo katika lugha. Inaeleza kuwa semantiki pia hujulikana kama *elimumaana*. Pia imeorodhesha aina mbalimbali za semantiki. Kwanza, kuna semantiki fafanuzi ambayo inachunguza maana za sentensi na semi zingine katika lugha. Pili, kuna semantiki leksika inayochunguza maana za tungo kwa kuzingatia zaidi kiwango cha neno ambapo pia utafiti huu unanuia kulenga. Tatu, inaorodhesha semantiki mantiki inayofafanua maana za sentensi na semi zingine katika lugha kwa kutumia vigezo vya kimantiki. Nne, kuna semantiki miundo inayochunguza maana za maneno katika muundo wa tungo za lugha inayohusika. Tano na mwisho, kuna semantiki nadharia inayohusika na uundaji wa nadharia za jumla za maana.

Kibiki na Malangwa (2012) wakiwanukuu Radford na wenzie (2002) wanaeleza kuwa maneno mengi katika lugha ni ya kipolisemia, na wanafafanua kuwa kadiri muda unavyopita maana tofauti huingizwa katika lugha na hivyo kusababisha maana za maneno kuongezeka au kubadilika. Wakifafanua zaidi suala la mabadiliko ya maana za maneno, wanawanukuu Ullmann (1957) pamoja na Wijaya na Yaniterzi (2011) na wanaeleza kuwa neno linaweza kutunza maana nyingine nyingi za ziada.

Maana hizi mpya huweza kupata mashiko zaidi na hivyo kutumiwa zaidi na wazungumzaji wa lugha kuliko ile maana ya msingi. Kwa kuwa maana ya lugha ilichunguzwa, utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa sitiari na metonimu katika uzuaji wa polisemia katika Kiswahili.

Polisemia ni sifa mojawapo ya kimsingi ya mfumo wa kileksika wa lugha. Polisemia ni hali ya neno kuwa na maana zaidi ya moja (Chacha na Pendo, 2019). Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2018), polisemi ni leksimu yenye maana mbili au zaidi zenye uhusiano, kwa mfano ‘kupe’ kwa maana ya mdudu ambaye hung’ang’ania kwenye miili ya wanyama na kuwafyonza damu na ‘kupe’ kwa maana ya mtu anayepata mapato bila kutumia jasho lake. Kwa hivyo, polisemia ni hali ambapo maneno huwa na maana zaidi ya moja na maneno hayo yanakuwa na uhusiano wa kihistoria. Mifano ya polisemi ni kama ifuatayo: neno ‘jicho’ litarejelea maana mbalimbali zinazohusiana kama jicho la mtu, jicho la viazi na jicho la sindano. Neno ‘mguu’ litarejelea maana kama vile, mguu wa binadamu au mguu wa meza au kiti. Hali hii huwepo kwa sababu kuna sifa fulani za kimsingi za kufanana

katika vitajwa viwili. Kwa mfano, kuna uhusiano baina ya “mdomo wa chupa” na “mdomo wa binadamu”.

Dhana ya sitiari ni ya kale, imekuwepo tangu enzi za Plato, Aristotle na Shakespere. Imezidi kujadiliwa na kuendelezwa na wataalamu mbalimbali kwa mfano, Chacha na Pendo (2019) wakimnukuu Kuhenga (1977) wanaeleza kuwa sitiari ni neno linalozaliwa kutokana na neno *sitiri* lenye maana ya kuficha au kufunika. Kwa hivyo, wanafafanua sitiari kuwa ni tamathali ya usemi ambayo inalinganisha vitu ama watu lakini bila kutumia viunganishi.

Naye Massamba (2004) anaeleza kwamba sitiari ni mbinu ambayo kitu au dhana inaelezwa kupitia dhana au kitu kingine kwa namna ya kukipa uzito kile kisemwacho. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2018), sitiari ni mchakato ambapo kitu kimoja kinahusishwa na kingine chenye sifa zinazofanana: kwa mfano, ‘mke wake ni chui nyumbani’ kumaanisha kuwa mke wake ni mkali akiwa nyumbani.

Kwa upande mwingine, metonimu ni tamathali ya usemi ambayo inatumika katika lugha ambapo kitu au dhana haitajwi kwa jina lake ila kwa jina la kitu au dhana nyingine inayohusiana nayo kwa karibu (Chacha na Pendo, 2019). Pia wanaendelea kueleza kuwa metonimu ni suala muhimu katika mabadiliko ya kisemantiki. Kiini cha uhamisho huwa ni kwamba tunatumia neno si tu fahiwa yake ya kawaida bali neno huhusishwa na muktadha wa kiuhusiano. Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza mchango wa sitiari na metonimu katika uzuaji wa polisemi.

1.1 Suala la utafiti

Polisemia ni hali ya neno moja kuhusishwa na maana zaidi ya moja. Mbinu za uzuaji wa polisemi ambazo zimejadiliwa ni: ukopaji, mabadiliko katika matumizi ya neno, ufasiri mpya wa homonimu na matumizi maalumu katika vitengo vya kijamii (Chacha na Pendo, 2019).

Sitiari ni mbinu au hali ambapo dhana moja inaelezwa kupitia dhana nyingine tofauti. Nayo metonimu ni mchakato ambapo neno au jina linatumiwa kurejelea kitu kingine ambacho kinahusiana na hicho cha kwanza kwa namna fulani. Michakato hii miwili inafanana kwa sababu inahusisha vitu viwili tofauti. Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi yaliyokolea ya sitiari na metonimu kwa namna ambavyo istilahi zote mbili zinaleta dhana mbili tofauti; bado si wazi mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia kuzua dhana ya pili kutoka kwa ya kwanza. Kwa hivyo, hayo yalibainishwa kupitia utafiti huu na kuonyesha namna sitiari na metonimu zinavyochangia kuzua polisemia. Pia sitiari na metonimu zinapoungana, kitu kimoja na kingine hakihusishi uzalishaji wa vipashio vipya vya kileksia, kifonolojia au kisintakisia bali hutumia rasilimali za isimu zilizopo.

1.2 Malengo ya utafiti

Utafiti huu ulitazamia kutimiza malengo yafuatayo:

1. Kubainisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu katika Kiswahili.
2. Kuainisha polisemi katika lugha ya Kiswahili.

3. Kudhihirisha mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia kuunda polisemi katika Kiswahili.

1.3 Maswali ya utafiti

Uchunguzi huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

1. Polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu ni zipi katika Kiswahili?
2. Polisemi huainishwaje katika lugha ya Kiswahili?
3. Ni mchakato upi ambao sitiari na metonimu hupitia kuunda polisemi katika Kiswahili?

1.4 Sababu za kuchagua mada

Kwa mujibu wa Creswell (2014), mada huchaguliwa baada ya kutafakari iwapo inaweza kutafitika. Mada ya utafiti huu ilichaguliwa na mtafiti kwa kuwa utafiti uliofanywa ulikuwa na mchango mkubwa katika kuikuza taaluma ya semantiki kidhana na kinadharia. Utafiti huu uliweka misingi ya njia mbalimbali zinazochangia uzuaji wa polisemi katika Kiswahili mbali na njia zilizopo. Kwa kufanya hivi, eneo la isimu na semantiki litapanuliwa kiusomi kwa kuwepo na tafiti tofauti na tafiti zaidi za siku zijazo.

Pia, kwa muda mrefu, sitiari na metonimu zimekuwa zikichunguzwa na kushughulikiwa zaidi katika eneo la fasihi kuliko kwenye uwanja wa semantiki. Hali hii imesababisha wasomi wengi kuwa na maoni kwamba vipengele hivi ni vya fasihi tu. Kwa hivyo, utafiti huu utakuwa muhimu kwa kuwa utawachochea wasomi kuanza kuangalia vipengele vingine vya fasihi kama vile lakabu, methali, tashbihi na jazanda namna ambavyo vinaweza

kuchangia kwenye semantiki. Kwa hivyo, kama hilo litaweza kushughulikiwa na wasomi basi uwanja wa isimu utaweza kupanuliwa zaidi.

Vilevile kazi yenyewe itawafaa wasomi na wataalamu wa Kiswahili kwa kuwa utafiti huu utapanua uelewa wao wa dhana ya sitiari, metonimu na polisemi. Pia matokeo ya utafiti unaokusudiwa kutekelezwa yatakuwa na umuhimu katika kuongeza maarifa katika taaluma ya semantiki.

1.5 Upeo na mipaka ya utafiti

Upeo ni kiwango ambacho sehemu ya utafiti itajikita nao na vipimo ambavyo vitatumika katika utafiti huo (Berg, 2001). Utafiti huu upeo wake ni maneno ambayo ni polisemi ambapo mtafiti alichunguza polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu katika lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Marshall na Rossman (1995), upeo katika utafiti waweza kuwa mpana au finyu kulingana na suala la utafiti na malengo ya utafiti. Ni bayana kuwa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)* ina maneno mengi kwa mfano, homografi, homonimu, sinonimu, antonimu na homofoni ila utafiti huu ulijikita katika polisemi ambazo ni sitiari na metonimu. Pia, utafiti huu ulijikita katika lugha ya Kiswahili kwa kupambanua namna sitiari na metonimu zinavyoweza kuzua polisemi katika Kiswahili.

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Yaliyoandikwa kuhusu mada yalihakikiwa katika vijimada vitatu ambavyo ni tafiti kuhusu polisemia, sitiari na metonimu.

1.6.1 Yaliyoandikwa kuhusu polisemia

Dhana ya polisemia imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali kwa mfano, Mapunda na Ngunguti (2021) waliandika makala kuhusu polisemia na usitiari wa ungonoshaji wa maneno katika Kiswahili cha mazungumzo. Katika utafiti wao walibaini kwamba ungonoshaji ni sitiari zaidi kuliko polisemia. Huu ni utafiti ambao unakaribiana na utafiti huu ijapokuwa utafiti wao ulijikita katika kipengele cha ungonoshaji.

Naye Mwendamseke (2016) aliandika makala kuhusu uelekeo wa maana za kipolisemia katika msamiati wa Kiswahili akitoa mifano kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Alitumia nadharia ya maana kama dhana ili kuafikia malengo ya utafiti huo. Katika utafiti wake, aliweza kubaini kuwa kuna baadhi ya maneno ambayo huwa na maana zaidi ya moja ambapo maana mpya ya neno fulani huhusishwa na maana msingi kwa njia fulani, na utokeaji wake upo wa aina tofauti. Kwa hivyo utafiti wake ni tofauti na ule ambao mtafiti alitekeleza. Tofauti hiyo ni kuwa, mtafiti alijikita kwa mchango wa sitiari na metonimu katika uzuaji wa polisemia katika Kiswahili.

Naye Masharipova (2020) amechunguza vipengele muhimu vya polisemia katika lugha za Kiingereza na Kiuzbeki. Katika makala yake alibaini aina za polisemia, vipengele muhimu vya kimuundo vya polisemia, tafsiri tofauti ya matumizi na uainishaji wa polisemia katika Kiingereza na Kiuzbeki. Utafiti wa Masharipova (2020) ulilenga uainishaji wa polisemia katika lugha mbili ambazo ni Kiingereza na Kiuzbeki. Utafiti ambao mtafiti alitekeleza nao

uliainisha polisemia ambazo zimezuka kutoka kwa sitiari na metonimu kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)*.

1.6.2 Yaliyoandika kuhusu sitiari

Tafiti mbalimbali zimefanywa juu ya sitiari, na miongoni mwa wasomi walioshughulikia sitiari ni Ndirangu (2011), aliyechunguza matumizi ya sitiari katika vitengo maalumu vya matangazo ya redio za kiasili nchini Kenya. Alieleza namna lugha ilivyotumiwa katika kipindi cha uchaguzi, kabla, wakati, na baada ya ghasia za uchaguzi katika mwaka wa 2007. Huu ni utafiti ambao ulibainisha jinsi sitiari zinafaa katika kuficha jambo au kitu kisijulikane au kisioneke kwa uwazi. Kwa upande mwingine, utafiti ulioteklezwa ni tofauti na wa Ndirangu. Huu ulijikita kwa mchango wa sitiari katika uzuaji wa polisemi katika Kiswahili.

Naye Gaichu (2016) alichunguza sitiari dhanifu katika methali za Kiswahili akitumia nadharia ya uhusiano. Katika utafiti wake alibainisha kuwa neno lililotumika kisitiari linapata maana linapokuwa kwenye matumizi yake au kwenye muktadha maalum. Maana ya neno lililotumika kisitiari inaweza kubadilika au ikabaki namna iyo hiyo. Kwa mfano, maana ya moja kwa moja ya sentensi kama *Kazija ni Ndumakuwili* haiwezi kuchukuliwa kama maana ya kitamathali itakuwa *Kazija ni mtu ajifanyaye mwema na rafiki, kumbe ni mwovu*. Ili kufasiri maana ya kitamathali ya sitiari, inabidi kwanza mtu ajue maana asilia ya sitiari na kisha ailinganishe na hali halisi ya maisha. Utafiti wa Gaichu (2016) ni tofauti na ule ulioteklezwa kwa vile utafiti wa Gaichu ulijikita kwa sitiari dhanifu katika methali za Kiswahili ilhali huu ambao

ulioteklezwa ulijikita katika polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari katika Kiswahili.

Kitundu na Malangwa (2020) walifanya utafiti kuhusiana na makala kuhusu ujenzi wa maana katika sitiari na tashibihi za Kiswahili. Katika utafiti wao ilibainika kuwa maana katika sitiari zinajengwa kutokana na mwingiliano wa sehemu tatu ambazo ni kuzungumzwa, kifananishwa na kiungo. Kwa mfano, katika sentensi *Hamza ni Chui*, kizungumzwa ni Hamza, kifananishwa ni chui na kiungo ni zile sifa na tabia za chui ambazo ni mtu mkali. Vilevile, ilibainika kuwa kuna kufanana na kutofanana kwa sitiari na tashibihi katika kuunda maana. Kwa hivyo, utafiti wao ulijikita kwa namna sitiari na tashibihi zinavyoingiliana katika ujenzi wa maana ilhali utafiti ulioteklezwa ulijikita kwa namna sitiari na metonimu zinavyoweza kuchangia katika uzuaji wa polisemi katika Kiswahili.

Naye Makame (2015) alichunguza jinsi maana za kisitiari zinavyojitokeza katika nomino za Kiswahili. Alibaini kuwa nomino za Kiswahili hupokea maana za kisitiari baada ya wazungumzaji kuhamisha sifa au dhana fulani kutoka kitu fulani hadi kingine. Utafiti wa Makame (2015) ulijikita katika jinsi maana za kisitiari zinavyojitokeza katika nomino za Kiswahili, tofauti na utafiti ulioteklezwa na mtafiti.

1.6.3 Yaliyoandikwa kuhusu metonimu

Metonimu ni neno au jina linalotumiwa kurejelea kitu kingine ambacho kinahusiana nacho kwa namna fulani. Kwa mfano, 'Nairobi' ni metonimu ya serikali ya Kenya (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu, 2018*). Pia, metonimu ni

tamathali ya usemi ambapo jambo au dhana haiitwi kwa jina lake lenyewe bali kwa jina la kitu kinachohusishwa kwa karibu na kitu hicho au dhana.

Metonimu imeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali kwa mfano, Zoltan (2013) aliyechunguza uhusiano wa sitiari na metonimu. Katika huo utafiti alibaini kuwa sitiari zenye msingi wa uwiano huibuka kutoka kwa viwakilishi vya kiakili kama fremu kupitia hatua ya kimetonimia. Alipendekeza kwamba hili hutendeka wakati kipengele kimojawapo cha muundo wa kiakili unaofanana na sura kinapojumlisha dhana ambayo iko nje ya fremu ya awali katika sehemu tofauti ya mfumo wa dhana. Kwa hivyo, utafiti wa Zoltan (2013) ni tofauti na ule uliotekelzwa kwa sababu utafiti uliofanywa ulichunguza namna metonimu inavyozua polisemi katika Kiswahili.

Naye McCasland (1949) alichunguza metonimu za *Agano Jipya* zinazomrejelea Mungu. Katika utafiti wake alibainisha metonimu mbalimbali zinazomrejelea Mungu kwa mfano, katika kitabu cha Luka sura ya 11:2, akawaambia, *msalipo semeni Baba (yetu aliye juu mbinguni)*. Metonimu ‘baba’ imetumiwa kumrejelea Mungu. Utafiti wa McCasland haukuonyesha namna metonimu zinavyoweza kuzua polisemi. Kwa hivyo, utafiti huo ni tofauti na utafiti uliotekelzwa.

1.7 Misingi ya nadharia

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya semantiki tambuzi. Katika sehemu hii, mtafiti alieleza nadharia ya semantiki tambuzi na mihimili yake. Pia, alionyesha namna mihimili ya nadharia ya semantiki tambuzi ilivyomsaidia kuhakiki kazi yake.

1.7.1 Nadharia ya semantiki tambuzi

Evans na Greens (2006) wanafafanua kuwa nadharia ya Isimu Tambuzi ilitokana na wanaisimu ambao walijitokeza katika miaka ya 1970 kutokana na kutokubaliana na wanaisimu hao wa kabla ya miaka ya 1970 kuhusu mitazamo ya lugha iliyokuwapo wakati huo. Nadharia ya Isimu Tambuzi imetokana na mchipuko wa sayansi tambuzi na fikira za awali za mwanafalsafa Gestalt pamoja na tafiti zilizohusu jinsi binadamu wanavyoainisha vitu. Nadharia ya Isimu Tambuzi ilizua nadharia kama vile nadharia ya sarufi tambuzi na nadharia ya semantiki tambuzi ambazo ni miongoni mwa nadharia ambazo zinashughulikia masuala ya uchunguzi wa lugha. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya semantiki tambuzi.

Edwin (2015), akimnukuu Geeraerts (2009), anaeleza kuwa nadharia ya semantiki tambuzi ilitokana na nadharia ya Isimu Tambuzi katika miaka ya 1980. Nadharia ya semantiki tambuzi ilipinga maelezo kuwa semantiki ilibuniwa baada ya sintaksia kama ilivyodaiwa katika nadharia zalishi za lugha. Kwa mujibu wa Lemmens (2017), semantiki tambuzi ni mtazamo unaochunguza uhusiano kati ya maumbo ya lugha, akili na maumbo yanayopatikana katika ulimwengu na jamii kwa ujumla.

Naye Gardensfors (1999) anafafanua kuwa semantiki tambuzi ni tofauti na semantiki halisia. Anaendelea kusema kuwa katika semantiki halisia, maana ya usemi hupatikana katika ulimwengu halisi. Katika semantiki tambuzi, maana ya usemi hulinganishwa na mifumo ya kiakili. Kwa hivyo, kulingana na nadharia hii, maana ya dhana si urejeleo wake kwenye kitu, wala uhusiano

wake na ulimwengu halisi bali maana hutokana na tajiriba aliyonayo mtu kuhusiana na kitu hicho au uhusiano wake na kitu hicho.

Pia, katika semantiki tambuzi, mkazo upo katika semantiki leksika. Maana iliyo muhimu hapa ni inayohusiana na dhana iliyo kichwani mwa binadamu kulingana na tajiriba yake. Miongoni mwa waitifaki wa nadharia ya semantiki tambuzi ni Lakoff (1987), Langacker (1987), na Lemmens (2017) wanaosema kuwa utaratibu wa uelewa wa binadamu hutokana na tajiriba zake za kimwili.

1.7.2 Mihimili ya nadharia ya semantiki tambuzi

Mtazamo huu una misingi ifuatayo: Maana hujikita katika kaida na tajriba aliyonayo mtu kuhusiana na kitu au uhusiano wa kitu hicho. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti katika kufafanua maana inayoletwa na lugha ya kiistiari na kimetonimu.

Maana huwa na muundo wa kiensaiklopedia. Gichuru (2020), akiwanukuu Greeraets (2006) na Lemmens 2017), anasema kuwa maana hujumuisha maana asilia pamoja na fahiwa zake zote. Kwa hivyo, mhimili huu una maana kuwa mtu akijua maanamsingi ya leksia pia anajua maana zingine na leksia hiyo katika matumizi yake. Mhimili huu ulimfaa mtafiti kuonyesha uhusiano uliopo kati ya polisemi fulani na maarifa yaliyohusishwa nazo katika jamii.

Lugha huhusisha ujenzi wa taswira za kimawazo na mipaka ya kidhahania katika mawanda ya kiutambuzi. Mhimili huu unasisitiza kwamba binadamu ana umilisi wa kuhamisha dhana mbalimbali kidhahania kupitia sitiari na

metonimu ili kupitisha ujumbe fulani. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti katika kueleza maana leksia inayoletwa na matumizi ya sitiari na metonimu.

Maana imejikita katika maumbile ya binadamu yakiwa msingi wa kufasiri dhana katika ulimwengu wake. Kulingana na Vyvyan na Greens (2006) na Lemmens (2017), maana haipo kwenye ishara au maumbo ya lugha bali inatokana na tajriba za pamoja za wanajamii zinazohusiana na umbile la binadamu. Mhimili huu ulimfaa mtafiti kwa sababu ulimsaidia katika kueleza tofauti mbalimbali zinazozuka kutokana na ufasiri wa dhana moja.

Maarifa ya kiutambuzi huwa katika kategoria zenye mizunguko na uzito wa maana kutoka kiinimaana. Gichuru (2020), akiwanukuu Vyvyan na Greens (2006), anaeleza kuwa leksimu ni kipashio kinachotumiwa na wasemaji katika kufikia ujuzi uliopo katika hifadhi ya maarifa katika utambuzi na masuala mengine yanayohusiana na dhana. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti katika kueleza namna maana mpya inavyozuka kutokana na maana ya kimsingi ya neno.

Maana ni kipashio kisicho thabiti ambacho hubadilika inapohitajika. Mhimili huu unaeleza kuwa maana hueleweka kwa ukamilifu ikiwa muktadha wa jamii inamotumika utazingatiwa. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti katika kueleza namna maana za leksimu zinavyoweza kueleweka kulingana na muktadha.

Uainishaji. Binadamu ana umilisi mkubwa wa kuainisha vitu mbalimbali ambapo vitu vyenye sifa sawa huwekwa pamoja. Mhimili huu ulimfaa mtafiti

katika kuainisha sitiari na metonimu katika makundi mbalimbali zilizochangia katika kuunda polisemi katika Kiswahili.

1.8 Mbinu za utafiti

Sehemu hii inajumuisha mbinu za utafiti zilizotumiwa ili kufanikisha utafiti huu. Mbinu hizi ni kama vile muundo wa utafiti, eneo la utafiti, usampulishaji, ukusanyaji wa data, maadili ya utafiti na uchanganuzi na uwasilishaji wa data ya utafiti.

1.8.1 Muundo wa utafiti

Utafiti ulioteklezwa ulichukua muundo wa kimaelezo ambapo maelezo yalitumiwa kutoa ufafanuzi wa polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu kulingana na malengo ya utafiti huu. Pia, majedwali yalitumika kuwasilisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana sitiari na metonimu ili ziweze kueleweka na kubainika wazi.

1.8.2 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta ambapo mtafiti alitembelea maktaba hii ili kusoma kazi zilizoandikwa kuhusu mada ya utafiti huu. Maktabani mtafiti alikusanya data kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)* ambapo mtafiti alidondoa polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu.

1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Mugenda na Mugenda (2019) wanadai kuwa sampuli inarejelea sehemu ndogo ya kitu inayochaguliwa katika vitu vingi kwa ajili ya kuwakilisha jumuiya nzima. Vilevile, sampuli ni sehemu ya idadi maalum ya watu ambayo mtafiti

atumia katika ukusanyaji wa data zitakazomsaidia kufikia malengo ya utafiti wake (Mugenda na Mugenda, 2003).

Creswell (2007) anadai kuwa sampuli ya kimakusudi ni aina ya sampuli iliyochaguliwa na mtafiti kwa misingi ya sifa anazozichunguzia katika kundi nzima yake. Nakubaliana na kauli ya Creswell (2007) kuhusu pambanua yake ya sampuli ya kimakusudi na kauli yake ilifaa katika utafiti uliotekelzwa. Mtafiti alitumia sampuli ya kimakusudi kuteua polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu kutoka kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)*. Sababu ya kuteua sitiari thelathini na metonimu thelathini ambazo zinachangia kuzua polisemi katika utafiti uliotekelzwa ni kutokana na kuongozwa na maoni ya Milroy (1987) ambaye anapendekeza matumizi ya sampuli ndogo katika uchunguzi wa lugha kwa kuwa sampuli kubwa inaweza kuzua data yenye urudufu mwingi.

Mugenda na Mugenda (1999) wanaeleza kuwa uteuzi wa sampuli ya kimakusudi unafaa katika utafiti wenye muundo wa kimaelezo ambao lengo lake kuu ni kupata habari au data kwa misingi ya malengo ya utafiti husika. Pia, ni kwa msingi huu, mtafiti aliteua sitiari arobaini na tano na metonimu kumi na tano ambazo zilichangia kuunda polisemi ambazo zilitumika katika kufanikisha utafiti huu.

1.8.4 Mbinu za ukusanyaji data

Kwa kuwa utafiti huu ulikuwa wa maktabani, mbinu zilizotumika ni usomaji na udondoaji.

Usomaji na udondoaji

Katika ukusanyaji wa data ya maktabani, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)* ilitumika. Mtafiti alidondoa polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu.

1.8.5 Uchanganuzi wa data

Katika hatua ya uchanganuzi, data ilipangwa kimfumo kutegemea malengo ya utafiti. Baada ya kukusanya na kupanga data, ilichaganuliwa kwa kutumia maelezo, michoro na majedwali katika misingi ya nadharia ya semantiki tambuzi.

1.8.6 Uwasilishaji wa matokeo

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya kinaelezo, michoro na majedwali. Michoro ilitumika kuwasilisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu ili kuonyesha mchakato ambao dhana hizo hupitia kuunda polisemi. Majedwali yalitumiwa kuwasilisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu ili ziweze kueleweka na kubainika wazi.

1.8.7 Maadili ya utafiti

Utafiti uliotekelezwa ulizingatia maadili ya utafiti kikamilifu. Mtafiti alihakikisha kuwa kazi zote zilizorejelewa katika utafiti huu zilijumuishwa katika sehemu ya marejeleo. Pia mtafiti alihakikisha kuwa utafiti huu ni kazi yake asilia na haijawahi kuwasilishwa katika chuo chochote nchini na nje ya nchi kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine. Mwisho

mtafiti aliomba idhini ya kufanya utafiti kutoka idara husika za utawala ili kufanikisha utafiti huu.

1.9 Hitimisho

Mambo ya kimsingi yameshughulikiwa katika sura hii, na imetoa mwelekeo na utaratibu uliofuatwa katika kushughulikia mada ya utafiti. Yaliyoshughulikiwa ni kama vile: usuli wa mada ya uchunguzi, suala la uchunguzi, malengo ya uchunguzi, maswali ya uchunguzi, upeo na mipaka ya utafiti, sababu za kuchagua mada ya utafiti, misingi ya nadharia ya semantiki tambuzi na mbinu za utafiti.

SURA YA PILI

POLISEMI AMBAZO ZIMEUNDWA KUTOKANA NA SITIARI NA METONIMU

2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumejadili polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu. Dhana ya polisemi imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali, baadhi ya wataalamu hao ni Chacha na Pendo (2019) wanaofasili polisemi kuwa ni leksimu yenye maana mbili au zaidi zenye uhusiano. Kwa mfano, neno ‘kupe’ kwa maana ya mdudu na ‘kupe’ kwa maana ya mtu anayeishi kwa kutegemea jasho la watu wengine. Ullmann (1967) anafasili polisemi kuwa ni sifa ya kimsingi katika mazungumzo ya binadamu ambapo licha ya kuwa na maana zaidi ya moja maana hizo huwa zina uhusiano.

Nayo sitiari ni mchakato ambapo dhana moja inaelezwa kupitia dhana nyingine tofauti. Hii ni mbinu kama tashbihi lakini ulinganishi huo haujitokezi waziwazi. Pia sitiari huhusisha vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile. Katika msingi huu, ni wazi kuwa sitiari kama zilivyo tamathali nyingi, imejengekea kwenye uhamishi wa maana. Metonimu ni tamathali ya usemi inayotumiwa katika lugha ambapo kitu au dhana haitajwi kwa jina lake ila kwa jina la kitu au dhana nyingine inayohusiana nayo kwa karibu. Metonimu hutokea kati ya maneno ambayo tayari yana uhusiano. Kwa hivyo sura hii imebainisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu katika lugha ya Kiswahili.

2.1 Polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari katika Kiswahili

Katika utafiti huu tuliweza kubainisha polisemi hamsini na tano za Kiswahili kutoka kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)* ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu. Kimsingi, polisemi huwa na kitomeo kimoja katika kamusi na maana zake hutengwa kwa namba za kawaida kama vile (1, 2, 3) ambazo hutumiwa katika utoaji wa maelezo ya maana zake husika. Kwa mfano, katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)*, polisemi huonyeshwa kama vile: **dhamira1** kiini cha jambo au habari iliyosimuliwa ama kuandikwa, hasa katika fasihi. **2** jambo analokusudia mtu kufanya. Nadharia ya semantiki tambuzi hueleza kuwa maana huwa na muundo wa kiensaiklopedia. Kwa hivyo, maana ya polisemi hujumuisha maana ya msingi pamoja na fahiwa zake zote. Kile ambacho nadharia hii inasisitiza ni kwamba maana ya polisemi fulani haiwezi kueleweka kikamilifu bila kuhusisha maarifa ya kiensaiklopedia ya polisemi hiyo. Polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari ni zifuatazo:

Bahari: Maana ya msingi ya neno ‘bahari’ ni eneo kubwa la maji ya chumvi linalozingira mabara na visiwa. Maana mpya ni kitu kikubwa. Tukichunguza maana ya awali na maana mpya ya leksimu ‘bahari’ tutabaini kuwa maana zote zimejikita katika kigezo cha ukubwa. Kwa mfano, “Juma na John wamekwenda Bahari ya Hindi kuvua samaki na papa.” Kauli hii imerejelea mahali mahususi ambapo Juma na John wamekwenda kuvua samaki. “Elimu ni bahari haina kuta wala dari” Hapa elimu imefananishwa na *bahari* kwa sababu elimu pia haina mwisho kama vile ambavyo bahari haina mwisho. Kwa hivyo, neno ‘bahari’ ni polisemi ambayo imeundwa kutokana na sitiari.

Beberu: Katika kamusi, maana za leksimu hii zimeorodheshwa zikiwa tano; (i) mbuzi dume (ii) mwanamume mwenye nguvu (iii) mtu anayetoa harufu mbaya (iv) taifa linalotawala nchi nyingine kiuchumi au kisiasa (v) mtu anayeamini na kutekeleza siasa ya ubeberu. Tukichunguza maana ya msingi ya leksimu ‘beberu’ (mbuzi dume) na maana mpya tutabaini kuwa kuna uhusiano wa kihulka kati ya maana hizo. Maelezo hayo yanaingiliana na mhimili wa semantiki tambuzi unaosisitiza kuwa binadamu ana umilisi wa kuhamisha dhana toka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine katika mawanda ya kiutambuzi. Kwa mfano, leksimu ‘beberu’ (mbuzi dume) imeakisi vitendo vya viongozi wabaya kama vile dhuluma, usumbufu na kero wanaowapa wenyeji kama afanyavyo mbuzi dume. Kimsingi, beberu ni mbuzi dume ambaye tangu utoto huwa hatulii, ana fujo zizi zima na mara nyingi hunuka kutokana na tabia yake ya kujikojolea. Kwa mfano, “John ni beberu katika jamii yake.” Sentensi hii ina maana kuwa John ni mtu mwenye nguvu au anayetoa harufu mbaya au pia mtu anayeeneza siasa ya ubeberu katika jamii yake. Kwa hivyo ni wazi kuwa leksimu ‘beberu imepanuka kisitiari kuunda polisemi.

Bawa: Maana ya msingi ya neno hili ni kiungo cha ndege au mdudu kimwezeshacho kuruka. Kutokana na fasili hii, ni wazi kuwa maana ya msingi imerejelea sehemu mojawapo ya ndege au mdudu inayomwezesha kuruka na kutua. Kwa mfano, “Ndege ana mbawa mbili zinazomwezesha kuruka na kutua.” Kwa upande mwingine, ni wazi kuwa maana ya msingi imepanuka kisitiari na kumaanisha kitu chochote kifananacho au kifanyacho kazi ya bawa. Kutokana na fasili hii, tunapata dhana kama vile; “bawa la eropleni.” Kwa hivyo ni dhahiri kuwa leksimu ‘bawa’ imepanuka kisitiari na kuunda polisemi.

Bomba: Neno hili lina maana sita kwenye kamusi ambazo ni: (1) aina ya mwanzi mpana na mrefu wa chuma, plastiki au saruji unaochimbiwa ardhini kupitisha mafuta au maji. (2) mwanzi unaotokeza juu ya paa la nyumba, karakana au melini ili kutoa moshi nje. (3) chombo cha kutilia dawa mwilini mwa binadamu au mnyama ili kutoa uchafu kama vile sikioni. (4) mtambo wenye mwanzi wa chuma, na kadhalika na shikio la kutoa maji sehemu ya chini kuenda sehemu ya juu kama vile kutoka kisimani. (5) chombo cha kusemea ili maneno yasikike mbali. (6) chombo cha kupulizia dawa ya majimaji ya kua wadudu. Tukichunguza fasili hizo tutabaini kuwa maana ya kwanza ya neno ‘bomba’ imepanuka kisitiari ambapo dhana ya ‘mwanzi’ inalinganishwa na vyombo mbalimbali kama vile chombo cha kupigia dawa ya mbu, chombo cha kusemea ili maneno yasikike. Pia utabaini kuwa dhana ya ‘mwanzi’ imehamishwa kwa sababu vyombo vyenyewe vina sifa hiyo ya kimsingi ya mwanzi. Kwa hivyo ni wazi kuwa neno ‘bomba’ limepanuka kisitiari kuunda polisemi.

Chiriku: Maana ya msingi ya neno ‘chiriku’ ni ndege mdogo mwenye kelele na maana mpya inayojitokeza ni mtu apendaye kusemasema. Kwa mfano, “kukiwa na *chiriku* mahali hutaweza kulala kwa kelele zao.” Kauli hii ina maana kuwa chiriku ni ndege wenye kelele sana. “Maria ni chiriku shuleni” ina maana kuwa, Maria ni mtu anayependa kupiga kelele akiwa shuleni. Hapa Maria amepewa sifa za chiriku kutokana na kupiga kelele kila mara shuleni. Vilevile maana ya awali ya leksimu ‘chiriku’ ina uhusiano na maana mpya kwa sababu zote zimejikita katika kigezo cha kelele. Kwa hivyo, ‘chiriku’ ni polisemi.

Chui: Maana ya msingi ya neno ‘chui’ ni mnyama kama paka lakini mkubwa. Kwa mfano, “Serikali ya Kenya imepiga marufuku uwindaji wa chui.” Maana mpya ni mtu mkali. Kwa mfano, “Maria ni chui nyumbani.” Kauli hii inamaanisha kwamba Maria ni mtu mkali akiwa nyumbani. Hata hivyo muktadha wa matumizi wa neno ‘chui’ katika sentensi hii unalenga maana ya ziada ambayo ni kuwa Maria si chui mnyama bali ana sifa za mnyama chui za kuwa na ukali. Kutokana na fasili hizo tumebaini kuwa maana ya msingi ya neno huhusishwa na maana mbalimbali. Pia tumebaini kuwa kuhusishwa kwa neno kunategemea aina ya jamii na matumizi ya neno fulani la kimsingi.

Dagaa: Maana ya awali ya leksimu hii ni samaki mwenye umbo dogo na aghalabu mwenye rangi inayong’aa. Kwa mfano, “Juzi kwa kina Riziki tulikula sima kwa mchuzi wa dagaa”. Maana mpya ni mtu au kitu cha kudharaulika. Kwa mfano, “Matatizo ni dagaa katika jamii yake.” Kauli hii ina maana kuwa Matatizo ni mtu ambaye amedharauliwa sana katika jamii yake. Kwa hivyo, leksimu ‘dagaa’ imechangia kuunda polisemi.

Dubu: Maana ya msingi ni mnyama mkubwa wa mwituni mwenye manyoya mengi. Kimsingi ‘dubu’ ni miongoni mwa wanyama wakubwa wawindaji na wala nyama. Pia, ni mnyama hatari na ni miongoni mwa wanyama wenye sifa za ukali. Kwa mfano, “Dubu wanaopatikana huko Antaktika ni wakali na wanaweza kumuua binadamu kwa urahisi.” Maana mpya ni mtu mpumbavu au baradhuli. Kwa mfano, “Musa ni dubu shuleni.” Kauli, “Musa ni dubu shuleni,” inamaanisha kuwa Musa ni mtu mpumbavu shuleni. Kutokana na

fasili hizo, tumebaini kuwa leksimu ‘dubu’ imepanuka kisitiari na kuunda polisemi.

Dubwana: Maana ya msingi ni kitu au mtu aliye na umbo kubwa lisilo la kawaida. Maana mpya ni kitu chochote kikubwa ambacho jina lake halijulikani. Kwa mfano, “Ndovu yule ni dubwana.” Hapa, ndovu amefananishwa na dubwana kutokana na umbo lake la ukubwa. “Tumbo ni dubwana nyumbani.” Sentensi hii ina maana kuwa Tumbo ni mtu ambaye ana umbo kubwa kuliko wengine nyumbani. Kwa hivyo tumebaini kuwa Tumbo amehusishwa na *dubwana* kutokana sifa zake za kiumbo zinazofanana na zile za *dubwana*.

Dimba: Leksimu hii ina maana tatu katika kamusi amabazo ni; (i) lango la kuingilia kumbini wanakokaa wari jandoni (ii) uwanja wa kumbini (iii) uwanja wa mpira kama vile wa miguu. Tukichunguza fasili hizo za leksimu ‘dimba’ ni wazi kuwa leksimu hii imepanuka kisitiari na kurejelea uwanja wa mpira. Kwa mfano, “Juma yuko dimbani.” (anacheza kandanda). Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa leksimu ‘dimba’ imechangia katika kuunda polisemi.

Fahali: Maana ya asilia ni ng’ombe dume na maana mpya ni mtu shujaa. Kwa mfano,

“Hamisi anao ng’ombe watatu na fahali mmoja.” Kauli hii ina maana kuwa kati ya ng’ombe wote wa Hamisi, fahali ni mmoja tu. “Amani ni fahali nyumbani.” Sentensi hii ina maana kuwa Amani ni jitu lenye maguvu mengi nyumbani. Kwa hivyo, hapa tunaona kuwa polisemi ‘fahali’ imeundwa kutokana na sitiari.

Firauni: Leksimu hii hurejelea jina la cheo cha wafalme wa zamani wa Misri. Kwa mfano, “Zamani za kale Misri ilitawaliwa na Firauni”. Maana ya pili ni mtu yeyote mwenye vitendo vichafu. Kwa mfano, “Nasaba Bora ni Firauni uongozini.” Sentensi “Nasaba Bora ni Firauni uongozini” ina maana kuwa Nasaba Bora ni mtu mwenye vitendo vibaya akiwa uongozini. Pia tumeona kuwa Nasaba Bora amefananishwa na *Firauni* kutokana na vitendo vyake vichafu kama vile vya Firauni. Hali hii inaingiliana na mhimili wa semantiki tambuzi unaodai kuwa binadamu ana uwezo mkubwa wa kuhamisha maarifa kutoka wanda moja la maarifa hadi jingine. Kwa hivyo, hapa tumeona kuwa sifa za wafalme wa zamani wa Misri zimehamishwa na kurejelea mtu mwingine. Vilevile, tumebaini kuwa neno ‘Firauni’ ni polisemi ambayo imeundwa kutokana na sitiari.

Fisi: Maana ya msingi ya leksimu ‘fisi’ ni mnyama wa mwituni mwenye ukubwa kama beberu, aliye na rangi ya kijivu na anayeaminiwa kuwa ni mwoga na anayependa sana kula mizoga. Kwa mfano, “Fisi ni mnyama mlafi sana alaye mizoga.” Maana mpya ni mtu mlafi. Kwa mfano, “Rose ni fisi karamuni.” Hapa Rose amepewa sifa za fisi kama vile za ulafi kulingana na tabia yake inayofanana na ile ya fisi. Kwa hivyo, tukichunguza maana ya msingi na maana mpya tutabaini kuwa maana hizo zina uhusiano ambapo maana zote zimejikita katika kitendo cha ulafi. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa leksimu ‘fisi’ imepanuka kisitiari kuunda polisemi.

Gwagu: Maana ya awali ni paka aliyeasi na kukimbilia porini. Maana mpya ni mtu mwovu. Kwa mfano, “Rose ni gwagu klabuni.” Kauli hii inamaanisha

kuwa Rose ni mtu mbaya akiwa klabuni. Hapa tumebaini kuwa leksimu ‘gwagu’ imepanuka kisitiari na kuchangia katika kuunda polisemi.

Hayawani: Maana ya msingi ni mnyama. Kwa mfano, “Haifai kuua *hayawani* porini ovyo kwani tukifanya hivyo tutakuwa tunayavuruga mazingira.” Maana mpya ni mtu asiye na ubinadamu; mtu asiye na haya wala adabu. Kwa mfano, “Maria ni hayawani nyumbani.” Hapa tunaona kuwa Maria amepewa sifa hii kutokana na tabia yake ya unyama kama ile ya hayawani. Kwa hivyo, ni wazi kuwa leksimu ‘hayawani’ imepanuka kisitiari na kuchangia katika kuunda polisemi.

Jambazi: Maana ya msingi ya neno ‘jambazi’ ni mwizi, hasa atumiaye silaha. Maana mpya ni mtu laghai na mjanja. Kwa mfano, “Jambazi likipatikana na hatia litanyongwa.” Kauli hii imerejelea maana ya msingi ya neno ‘jambazi’. Pia kwenye kamusi neno ‘jambazi’ ni polisemi. Kutokana na neno hili, tunapata sitiari “John ni jambazi, haaminiki asilani.” Kauli hii inamaanisha kuwa John ni mtu ambaye ni laghai, mwongo au mdanganyifu. Pia, imebanika kuwa John amehusishwa na jambazi kutokana na sifa zake zinazofanana na zile za *jambazi* kama vile uongo, udanganyifu na wizi. Kwa hivyo, tumebaini kuwa neno ‘jambazi’ limepanuka kisitiari kuunda polisemi.

Jogoo: Maana ya msingi ya neno ‘jogoo’ ni kuku dume. Maana mpya ni shujaa, mshindi, hodari. Kwa mfano, “Jogoo likiwika saa kumi mimi huwa nimekwisha amka”. “Hamni ni jogoo, haogopi kupambana na majambazi wa mjini.” Sentensi “Hamni ni jogoo, haogopi kupambana na majambazi wa mjini” ina maana kuwa Hamni ni mtu mwenye nguvu nyingi na pia si mwoga.

Kutokana na maelezo hayo, tumebaini kuwa neno ‘jogoo’ limepanuka kisitiari kuunda polisemi.

Jino: Leksimu hii ina maana tatu ambazo ni: (i) kipande kigumu cheupe kilicho kinywani mwa binadamu au mnyama kinachotumiwa kutafunia chakula au kukata vitu (ii) kitu kinachofanya kazi kama jino la mtu kinachotumika kwa kukatia, kutafunia au kushikilia vitu vingine (iii) ugonjwa wa meno au ufizi. Tukichunguza fasili za leksimu ‘jino’ tutabaini leksimu ‘jino’ imelinganishwa na kitu chochote kinachofanya kazi kama jino la mtu. Kutokana na maelezo hayo tunapata dhana kama vile, “jino la msumeno.” Kwa hivyo, ni wazi kuwa leksimu ‘jino’ imepanuka kisitiari na kuzua polisemi.

Jini: Maana asilia ya neno hili ni kiumbe asiyeonekana anayefikiriwa kuwa anadhuru watu. Fasili hii inaakisi iblisi au shetani. Kwa mfano, “Usishindane naye yule jini, mwache atakavyo.” Maana mpya ni mtu mwenye vitimbi; mtu mwovu. Kwa mfano, “Humwezi yule jini, atakalo lazima afanye”. Kwa hivyo kutokana na maelezo hayo ni wazi kuwa neno ‘jini’ limepanuka kisitiari na kuunda polisemi.

Jicho: Katika kamusi, maana za neno hili zimeorodheshwa zikiwa tatu; (i) kiungo cha mwili cha kuonea. (ii) panda liwekwalo katika gubeti ya jahazi. (iii) chipukizi la ua. Tukichunguza kwa makini fasili za leksimu ‘jicho’ tutabaini kuwa maana hizo mpya zina uhusiano wa kiumbo na maana ya msingi ambayo ipo katika namba moja. Pia, tulibaini kuwa maana ya msingi leksimu ‘jicho’ imepanuka kisitiari na kuwasilisha dhana nyingine kama vile jicho la viazi, jicho la sindano na jicho la mihogo.

Kasuku: Maana za kamusi za neno ‘kasuku’ ni ndege mkubwa mwenye rangi nyingi anayeweza kuiga kusema kama binadamu na mara nyingi hufugwa majumbani. Kwa mfano, “Kasuku wetu ubishapo atakukaribisha, kisha akuulize: Habari za leo?” Maana mpya ni mtu mwenye tabia ya kusema maneno mengi aghalabu kwa kuiga bila umakini. Kwa mfano, “Kazija ni kasuku nyumbani.” Katika sentensi “Kazija ni kasuku nyumbani”, Kazija amepewa jina la kasuku kutokana na sifa zake za kusema maneno mengi aghalabu kwa kuiga. Pia, ni wazi kuwa situari ‘kasuku’ imeweza kuchangia katika uundaji wa polisemi.

Kiboko: Maana ya msingi ni mnyama mkubwa na mnene anayeishi kwenye maji baridi na maana ya pili ni mtu mnene. Kwa mfano, “Tahadharini mnapoogelea ziwani, kuna mamba na viboko.” Sentensi “Tabu ni kiboko katika familia yao” ina maana kuwa Tabu ni mtu mnene kuliko wengine katika familia yao. Vilevile, Tabu amepewa sifa hii kutokana na kuwa na mwili mkubwa. Hapa, tukichunguza maana za leksimu ‘kiboko’ tutabaini kuwa kuna uhusiano wa kiumbo kati ya maana hizo. Pia leksimu ‘kiboko’ imepanuka kisitari na kuzua polisemi.

Kikohozi: Maana ya msingi ni ugonjwa wa kifua ambao humfanya mtu akohoe sana na kutoa balaghamu. Kwa mfano, “Kazija ana kikohozi.” Kauli hii inamaanisha kuwa Kazija anaumwa kifua. Maana ya pili ya leksimu ‘kikohozi’ ni hali ya kuingiwa moyoni na kuthamini mtu au kitu zaidi ya mwingine au kingine. Kwa mfano, “Maria ni kikohozi cha Hamza.” Sentensi “Maria ni kikohozi cha Hamza” ina maana kuwa Maria ni mtu ambaye amethaminiwa

sana na Hamza. Kwa hivyo, tumebaini kuwa leksimu ‘kikohozi’ imepanuka kisitiari na kuchangia katika kuunda polisemi.

Kupe: Maana ya awali ya neno ‘kupe’ ni mdudu ambaye hung’ang’ania kwenye miili ya wanyama na kuwafyonza damu. Kwa mfano, “Ng’ombe wa yule maskini wamejaa *kupe* mwilini”. Leksimu ‘kupe’ imebadilika kwa kupanuka kisitiari na kutumika kumaanisha mtu anayepata mapato au matunda bila ya kutumia jasho lake. Hii kwa hakika ndiyo tabia aliyo nayo kupe ya kufyonza na kunyonya damu za viumbe wengine. Kwa mfano, “Hamisi ni kupe kazini.” Kauli, hii ina maana kwamba Hamisi ni mtu anayetegemea wengine ili apate chakula na mahitaji mengine. Kwa hivyo, tumebaini kuwa neno ‘kupe’ limepanuka kisitiari na kuchangia kuunda polisemi.

Kinyonga: Maana asilia ya neno hili ni mnyama mdogo anayebadilika rangi ya mwili wake ili ifanane na rangi ya mazingira alimo na maana mpya ni mtu wa kubadilikabadilika; kigeugeu. Tukichunguza maana hizi tutabaini kuwa maana asilia ya leksimu ‘kinyonga’ imerejelea mnyama ambaye ni lumbwi. Kwa mfano, “Kinyonga ni mnyama anayeweza kujigeuza rangi tofautitofauti kulingana na mazingira yake.” Kwa upande mwingine, maana mpya nayo imerejelea binadamu. Kwa mfano, “Maria ni kinyonga sokoni.” Kauli hii inaashiria kuwa Maria ni mtu asiyekuwa na msimamo thabiti. Kwa hivyo, neno ‘kinyonga’ limepanuka kisitiari kuunda polisemi.

Kigoda: Maana asilia ya neno hili ni kiti kidogo, aghalabu cha miguu mitatu, kisichokuwa na kiegemeo. Kwa mfano, “Huko shamba, babu hana makochi na viti, bali hutumia vigoda kukalia ukumbini na barazani.” Maana mpya ya neno

‘kigoda’ ni jukwaa, aghalabu katika chuo kikuu, linaloanzishwa kwa lengo la kutambua na kuendeleza mawazo na falsafa ya mtu fulani. Kwa mfano, “Nchini Tanzania kuna kigoda cha Mwalimu Nyerere katika Idara ya Kiswahili.” Kutokana na maelezo hayo ni wazi kuwa neno ‘kigoda’ limepanuka kisitiari na kuchangia katika uzuaji wa polisemi.

Lango: Maana ya awali ya neno hii ni eneo lililo katikati ya nguzo mbili katika pande mbili zinazotazamana na uwanja ambapo sharti mpira uingie ili kuhesabu goli au bao: Kwa mfano, “Kulitokea msongamano katika lango la timu ya Yosa.” Maana mpya ya neno ‘lango’ ni mlango mkubwa unaotumika kuingilia ndani ya uwanja, mji, ngome na kadhalika. Nadharia ya semantiki tambuzi hueleza kuwa binadamu ana ujuzi mkubwa wa kuhusisha dhana zinazolingiliana kwa kutumia msingi wa maumbile. Ndiposa popote palipo na mahali pa kuingilia binadamu huhusishwa na lango. Kwa mfano, Dar es salaam ni lango la kuingilia Afrika Mashariki. Kwa hivyo leksimu ‘lango’ imepanuka kisitiari na kuunda polisemi.

Malaika: Maana ya msingi ya leksimu hii ni kiumbe asiyeonekana ambaye anasadikiwa kuwa ameumbwa na Mungu kwa nuru. Maana mpya ni mtoto mchanga. Kwenye kamusi, neno *malaika* ni polisemi. Kutokana na leksimu ‘malaika’ tunapata sitiari kama vile, “Rehema ni malaika nyumbani.” Kutokana na maana ya msingi ya neno ‘malaika’ tunapata mfano kama vile, “Malaika hawaonekani, lakini tunaamini wana kazi ya kumtumikia Mola.” Sentensi “Rehema ni malaika nyumbani” ina maana kuwa Rehema ni mtoto mchanga na

kwa hivyo hawezi kumaizi jema wala ovu. Pia, tumebaini kuwa neno ‘malaika’ limepanuka kisitiari ili kuchangia kuunda polisemi.

Mguu: Maana ya msingi ya leksimu hili ni kiungo cha mwili wa binadamu, mnyama au mdudu kinachomwezesha kusimama au kwenda. Kwa mfano, “Hakuna mtu anayeweza kutembelea kwa *mguu* mmoja.” Maana mpya ya leksimu ‘mguu’ ni kitu chochote kinachofanya kazi kama mguu. Kutokana na fasili hizo za hapo juu ni wazi kuwa maana ya leksimu ‘mguu’ imepanuka kisitiari na kuwasilisha dhana nyingine kama vile, “mguu wa meza” na “mguu wa kiti.” Hapa, tumebaini kuwa leksimu ‘mguu’ imefananishwa na vitu vingine vinavyofanya kazi kama hiyo ya mguu.

Mzinga: Katika kamusi, maana za neno hili zimeorodheshwa zikiwa nne; (i) kitu kirefu aghalabu cha mviringo chenye uwazi ndani kinachotengenezwa kwa mbao au mti. (ii) chombo kinachotengenezwa kwa chuma chenye mwanzi mkubwa ambao hutumika kurushia risasi kwa nguvu zaidi na mbali zaidi kuliko bunduki. (iii) idadi ya ushindi wa mabao sita katika mchezo wa karata. (iv) fremu ya ngoma ambayo huwambwa ngozi. Kutokana na fasiri hizo ni wazi kuwa maana za neno ‘mzinga’ zina uhusiano kwa namna fulani. Maana ya (i), (ii) na (iv) zina sifa ya kimsingi (kifaa chochote chenye mviringo). Pia neno ‘mzinga’ limetumika kisitiari kuwasilisha kitu hodari. Kwa mfano, “Ali ni mzinga katika karata.” Kwa hivyo ni dhahiri kuwa neno ‘mzinga’ limetumika kuunda polisemi.

Mtemi: Katika kamusi, leksimu hii ina maana mbili; (i) Mtawala wa kijadi. Kwa mfano, “Nchini Tanganyika kabla ya ukoloni kulikuwa na mtemi, ambaye

ni mtawala wa kienyeji.” (ii) mtu mwenye nguvu na hodari kwa kupiga wenziwe. Leksimu *mtemi* kwenye kamusi ni polisemi. Kutokana na leksimu ‘mtemi’ tunapata sititari “Juma ni mtemi nyumbani.” Kauli hii inaashiria kuwa Juma labda ni mtu mwenye nguvu au pia ni hodari kwa kuwapiga wenziwe akiwa nyumbani.

Mlango: Maana ya msingi ya leksimu hii ni uwazi au nafasi maalum iliyo ukutani ili kuingilia na kutokea mahali penye uwazi zaidi. Fasili hii inaakisi mahali pa kuingilia na pa kutokea kama vile nyumba. Kwa mfano, “Tunapolala usiku, mlango wa nyuma tunaufunga kwa ndani.” Kwa upande mwingine, maana ya msingi imepanuka kisitari na kumaanisha kizuizi kilichotengenezwa kwa ubao, chuma au kitu kingine chochote ili kuziba uwazi wa kuingilia na kutokea kwenye ukuta au kiambaza cha jengo, chumba au gari. Nadharia ya semantiki tambuzi husisitiza kuwa maumbile ya binadamu humsaidia kufasiri maumbo mbalimbali katika ulimwengu wake. Anapokumbana na umbo lolote linalofanana na mlango huhamisha maarifa aliyonayo hadi kwa dhana mpya. Ndiposa tunapata dhana kama vile, “mlango wa gari”, “mlango wa ndege” na “mlango wa behewa”.

Ndumakuwili: Maana ya msingi ya leksimu ‘ndumakuwili’ ni kiumbe afananaye na nyoka anayesemekana kuwa ana vichwa viwili. Kwa mfano, “Sijawahi kuona ndumakuwili ingawa wawindaji wengi husema wamepata kuwaona.” Maana mpya ni mtu ajifanyaye mwema na rafiki, kumbe yu mwovu. Kwa mfano, sentensi “Ali ni ndumakuwili shuleni.” Kutokana na fasiri hizi, Ali anasemekana kuwa ndumakuwili. Hii inatokana na tabia yake ya

kutokuwa na msimamo. Akienda kwa mtu A humsema vibaya mtu B na akienda kwa mtu B anamsema vibaya mtu A. Tabia ya Ali inafananishwa na tabia ya ndumakuwili ambaye anauma kila upande. Kwa hivyo, tumebaini kuwa leksimu ‘ndumakuwili’ imepanuka kisitiari kuchangia kuunda polisemi.

Nyonyo: Maana ya msingi ni ncha ya titi. Kwa mfano, “Mama humpa mtoto wake maziwa kwa kumpa nyonyo anyonye.” Maana mpya ambayo inajitokeza ni mpira mfano wa chuchu anaobembelezewa mtoto mchanga asilie au unaotiwa maziwa kwa ajili ya mtoto kunyonya. Hapa maana ya msingi imerejelea sehemu mahususi ya titi. Maana ya leksimu ‘nyonyo’ imepanuka kisitiari na kuwakilisha mpira mfano wa chuchu ambao kiumbo hufanana na ncha ya titi. Hali hii inaingiliana na mhimili wa nadharia ya semantiki tambuzi unaosisitiza kuwa maumbile ya binadamu humsaidia kufasiri maumbo mbalimbali katika ulimwengu wake. Maana huumbika kutokana na tajriba za binadamu zinazohusiana na umbile lake.

Nyundo: Maana msingi ya leksimu hii ‘nyundo’ ni kifaa kinachotumika kugongomelea katika shughuli kama vile za ujenzi, useremala au fundi. Kwa mfano, “Nyundo ya fundi yule mrefu hugongomelea msumari vyema.” Maana mpya ni mtu mfupi sana. Kwa mfano, “Maria ni nyundo shuleni.” Sentensi hii ina maana kuwa Maria ni mtu mfupi shuleni. Kwa hivyo tumebaini kuwa leksimu ‘nyundo’ imepanuka kisitiari na kuzua polisemi.

Nyonya: Maana ya awali ya neno hili ni vuta kitu kiowevu kwa mdomo au kwa kutumia mrija. Fasili hii inaakisi kitendo cha kunyonya kama afanyavyo mtoto anaponyonya maziwa. Kwa mfano, “Mtoto mchanga akilia mama

atamnyonyesha maziwa yake.” Maana ya msingi imepanuka kisitiari na kumaanisha kuishi kwa kutegemea mwingine bila ya kufanya kazi. Kwa hivyo, tabia hii imefananishwa na tabia ya mtoto kumtegemea mama yake bila kufanya kazi. Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa neno ‘nyonya’ limechangia katika kuunda polisemi.

Programu: Leksimu hii ina maana nne katika kamusi ambazo ni; (i) mpango wa mambo ambayo mtu au kampuni inakusudia kuyafanya (ii) mfumo wa kompyuta ulioandaliwa kwa ajili ya kutenda kazi fulani kama vile kuandaa bili, kutengeneza vitabu au kupeleka na kupokea baruapepe. (iii) kipindi katika televishini au redio (iv) masomo yanayofundishwa katika ngazi fulani ya elimu aghalabu chuo kikuu. Tukichunguza maana ya msingi ya leksimu ‘programu’ tutabaini kuwa maana hiyo imepanuka kisitiari na kuwakilisha masomo yanayofundishwa katika chuo kikuu. Kwa mfano, “programu za uzamivu” na “programu za uzamili.”

Shingo: Maana ya msingi ni sehemu ya mwili inyounganisha kichwa na sehemu zingine za mwili. Kwa mfano, “Shingo yangu inaniuma kwa kuubeba mzigo wa rafiki yangu kichwani.” Maana mpya ni sehemu yoyote nyembamba ya chupa inayounganisha mdomo wa chupa na sehemu yake nyingine. Wanasemantiki tambuzi hufafanua kuwa maumbile ya kipekee ya binadamu humwezesha kufasiri maumbo mbalimbali katika ulimwengu wake halisi. Anapopatana na umbo lolote linalofanana na ‘shingo’ ya mtu, huhamisha maarifa aliyo nayo hadi nyanja hiyo nyingine. Hapa, leksimu ‘shingo’

imepanuliwa kisitiari na kuwakilisha sehemu yoyote nyembamba iliyoko baina ya vitu.

Shume: Maana asilia ya neno hili ni paka mwizi asiyekaa nyumbani. Kwa mfano, “Babu alimuua paka shume jana usiku.” Maana ya pili ni mtu mwenye vitendo viovu. Leksimu ‘shume’ imepanuka kisitiari na kumaanisha mtu mwenye vitendo viovu. Kwa mfano, “Masumbuko ni shume nyumbani.” Hapa, Masumbuko amefananishwa na ‘shume’. Kwa hivyo, kuna uwezekano akawa mtu anayehusika ana sifa kadha zinazofanana na za paka shume kama za wizi. Tukichunguza fasili za leksimu hiyo na mifano iliyotolewa tutabaini kuwa, leksimu ‘shume’ imechangia katika kuunda polisemi.

Sungura: Maana ya msingi ya leksimu ‘sungura’ ni aina ya mnyama mdogo kama paka ambaye miguu yake ya nyuma ni mirefu kuliko ya mbele, mwenye mkia mfupi na masikio marefu, ambaye huchimbua ardhini, hula majani na huenda kasi kwa kurukaruka. Kwa mfano, “Mtoto yule amemkamata sungura leo.” Maana mpya ni mtu mjanja na mwerevu. Kwa mfano, sentensi “Juma ni sungura shuleni” ina maana kuwa Juma ni mtu mjanja akiwa shuleni. Hii inatokana na hali aliyo nayo Juma -hali ya ujanja. Katika jamii nyingi za kiafrika sungura (mnyama) husemekana kuwa mjanja sana kuwazidi wanyama wengine. Hali hii inaingiliana na mhimili wa nadharia ya semantiki tambuzi unaosisitiza kuwa maana hujikita katika utamaduni na tajriba za pamoja za wanajamii. Kwa hali hiyo, mtu yeyote ambaye anaonekana kuwa na hali ya ujanja huitwa sungura. Kwa hivyo leksimu ‘sungura’ imepanuka kisitiari kuunda polisemi.

Tako: Maana ya msingi ya leksimu ‘tako’ ni sehemu ya nyuma ya mwili baina ya kiuno na paja inayotumika kukalia. Kwa mfano, “Ukiwa na jipu la takoni utashindwa hata kukaa kitini.” Maana ya pili ya leksimu ‘tako’ ni sehemu ya chini ya kitu ambacho hutumiwa aghalabu kuwa kikalio. Tukichunguza maana za leksimu ‘tako’ zote zinarejelea sehemu ya chini hasa ambayo huwa ni kikalio, kwa hivyo maana hizi zina uhusiano. Pia, maana ya leksimu ‘tako’ imepanuka kisitiari na kurejelea dhana kama vile, “tako la bunduki”, “tako la bakuli” na “tako la sahani”.

Tawi: Neno hili lina maana mbili kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)* ambazo ni; (i) Sehemu ya mti inayoota kutoka shinani aghalabu hutoa majani na matunda. Kwa mfano, “Wananchi hawapaswi kukata hata tawi moja la mti bila ruhusa ya chifu ama afisa wa msitu.” (ii) Sehemu au ofisi ndogo ya chama, shirika, na kadhalika. Tukichunguza maana ya msingi na maana mpya, tutabaini waziwazi kuwa zina uhusiano kwa vile maana zote zinarejelea sehemu ya kitu. Nadharia ya semantiki tambuzi hueleza kuwa binadamu ana tajiriba kubwa ya kuhamisha ujuzi kutoka wanda moja la maarifa hadi jingine kupitia sitiari. Kwa mfano, maana ya leksimu ‘tawi’ imepanuka kisitiari na kurejelea dhana kama vile, “tawi la chama” na “tawi la chuo”.

Tata²: Maana ya msingi ni fundo katika uzi. Maana hii imeakisi hali ya uzi inapokuwa na mafundo. Kwa mfano, “Uzi umetata, acha niutatue, ili niweze kuutumia kushonea.” Maana ya msingi imepanuka kisitiari na kurejelea hali ya kutoeleweka, kufumbua au kufungwafungwa, kuwa na maana zaidi ya moja. Pia katika taaluma ya semantiki, leksimu ‘tata’ imepata maana maalumu na

kutumika kuelezea hali ya neno au sentensi kuwa na maana nyingi hivi kwamba inapotamkwa hatufahamu moja kwa moja maana iliyokusudiwa. Kwa mfano, “Niitie watoto wale.” Maana zinazojitokeza ni hizi: (a) wale chakula. (b) wale kama kionyeshi. Kwa hivyo ni wazi kuwa maana ya msingi ya hiyo leksimu imepanuka kisitiari na kuunda polisemi.

Tanua: Maana ya msingi ni vuta huku na huku ili kuongeza nafasi. Kwa mfano, “Juma ametanua miguu.” Maana mpya ni tutumua kitu ili kuongeza nafasi. Kutokana na fasili hizo tumebaini kuwa, leksimu ‘tanua’ imepanuka kisitiari kuleta maana ya kujigamba. Kwa mfano, “watu wanaojitanua huwa na sifa za kujigamba na kujiongezea sifa ambazo pengine hawana. Leksimu ‘tanua’ imechangia katika kuunda polisemi.

Ulimi: Leksimu hii katika kamusi, ina maana tatu ambazo ni; (i) Kiungo cha mwili ndani ya kinywa kinachotumika kwa kuonjea, kusemea, kurambia, na kadhalika (ii) Kitu chochote kinachofanana na ulimi (iii) shungi la miali ya moto hasa inapoonekana kwa mbali. Tukichunguza kwa makini maana hizo zina uhusiano wa kiumbo ambapo maana ya msingi imepanuka kisitiari na kuzua dhana mpya. Kutokana na maana mpya ya leksimu ‘ulimi’ tunapata dhana kama vile, “ulimi wa plau” na “ulimi wa moto.” Nadharia ya semantiki tambuzi husisitiza kuwa maumbile ya binadamu humwezesha kufasiri maumbo mbalimbali katika dunia yake. Anapokumbana na umbo lolote linalofanana na ulimi huhamisha maarifa aliyonayo kukabili dhana mpya. Ndiposa tunapata dhana kama vile, “ulimi wa plau” na “ulimi wa moto” kama ilivyoelezwa hapo juu.

Kutokana na utafiti huu tumebaini kuwa polisemi zilizoundwa kutokana na sitiari huonesha maana nyingi zenye etimolojia moja. Kwa hivyo, sitiari ni mfumo wa maana unaoangaza nje; yaani kitu katika nyanja moja huchukua mahali pa kingine katika nyanja tofauti kana kwamba vitu hivyo vinalingana. Pia, imebainika kuwa leksimu nyingi za kimsingi, yaani zinazotaja sehemu za mwili, wanyama na ndege zimepanuka kisitiari kuwasilisha dhana nyingine. Vilevile, uchunguzi wetu ulidhihirisha kuwa baadhi ya sitiari zinazounda polisemi zilijitokeza ndani ya homonimu. Kwa mfano, tata².

2.2 Polisemi ambazo zimeundwa kutokana na metonimu katika Kiswahili

Dhana ya metonimu imejadiliwa na wataalamu mbalimbali, mmoja wa wataalamu hao akiwa Bynon (1977) anayeeleza metonimu kuwa ni hali ambapo dhana pana ya lugha huwakilisha dhana finyu. Kwa mfano, leksimu ‘serikali’ hutumiwa kama metonimu ya ‘polisi’. Ni kawaida kusikia polisi wakisema “mwizi yuko mikononi mwa serikali”. Katika hali hii, leksimu ‘serikali’ imetumika katika nafasi ya polisi. Kwa hivyo, dhana pana (serikali) imetumika kuwasilisha dhana finyu (polisi).

Chacha na Pendo (2019) wanafasili metonimu kuwa ni tamathali ya usemi inayotumiwa katika lugha ambapo kitu au dhana haitajwi kwa jina lake ila kwa jina la kitu au dhana nyingine inayohusiana nayo kwa karibu. Kwa mfano, ‘Westminister’ ni metonimu ya Bunge la Uingereza. Kwa upande mwingine, Mbatiah (2001) anaeleza kuwa japo fahiwa ya metonimu huangaziwa katika semantiki, fahiwa hii pia hutumiwa na wanafasihi ambapo fasili yake hutokana na kutajwa kwa sifa ya kitu ili kudokeza maana kusudiwa badala ya kitu

chenyewe. Kwa hivyo, kutokana na maelezo hayo, metonimu ni mchakato ambapo neno au jina linatumiwa kurejelea kitu kingine ambacho kinahusiana na hicho cha kwanza kwa namna fulani. Polisemi ambazo zimeundwa kutokana na metonimu ni zifuatazo;

Bloku: Maana asilia ya neno hili ni pande kubwa kama vile la tofali, mti, jiwe aghalabu lenye umbo mraba ama bapa kila upande. Kutokana na fasili hii tunapata dhana kama vile “nyumba ya matofali.” Kwa upande mwingine, maana mpya ni jengo kubwa la ghorofa lenye mgawanyiko wa nyumba, maduka, ofisi na kadhalika. Kwa mfano, “Mwinyi aliuza bloku lake jana.” Kutokana na maelezo haya tumebaini kuwa neno ‘bloku’ limetumiwa kuwakilisha ‘jengo kubwa la ghorofa’. Pia ni wazi kuwa neno ‘bloku’ limechangia katika kuunda polisemi.

Bunge: Maana ya awali ya neno hili ni baraza la taifa la kutunga sheria na lenye wajumbe waliochaguliwa na wananchi ili kuwakilisha. Kwa mfano, “Bunge la taifa la Uganda litakongamana kesho jioni.” Leksimu hii pia hutumiwa kumaanisha ‘wawakilishi wa maeneo ya bunge wanaokaa bungeni’. Kwa mfano, Bunge limesema kuwa halitashinikizwa kutunga sheria. Kwa hivyo, ni wazi kuwa leksimu ‘bunge’ imepanuka maana na kuwakilisha dhana nyingine.

Choo: Maana ya msingi ya leksimu hii ni mahali pa kwenda haja. Kwa mfano, “Ukiwa na haja, choo kiko hapo nyuma ya nyumba.” Maana mpya ya leksimu ‘choo’ ni kinyesi. Kwa mfano, “Majeruhi alitokwa na choo baada ya kunusurika chupuchupu ajalini.” Kwa hivyo, leksimu ‘choo’ imetumiwa kama

metonimu ya ‘kinyesi’ ambapo dhana pana (chumba) imetumika kuwakilisha dhana finyu (kinyesi). Hali hii inaingiliana na mhimili wa nadharia ya semantiki tambuzi unaosisitiza kuwa binadamu ana tajiriba kubwa ya kuhamisha ujuzi kutoka wanda moja la maarifa hadi jingine ambapo leksimu *choo* imehamishwa na kuwakilisha ‘kinyesi’. Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa leksimu ‘choo’ imechangia katika kuunda polisemi

Chuo¹: leksimu hii ina maana tatu katika kamusi ambazo ni; (i) asasi inayotoa mafunzo maalumu ya kazi fulani: ~ cha Ufundi; ~ cha Kilimo; ~ Ualimu. (ii) mahali watu wanapojifunza Kurani. (iii) kitabu cha dini cha Kiislamu kilichoandikwa na mtu kwa hati za Kiarabu. Kutokana na fasili hizo, ni wazi kuwa leksimu ‘chuo¹’ imetumiwa kumaanisha ‘kitabu’ ambapo dhana pana (chuo¹) imetumika kuwasilisha dhana finyu ‘kitabu cha dini cha kiislamu kilichoandikwa na mtu kwa hati za Kiarabu.’ Kwa mfano, “Shehe alinunua chuo¹ chake jana.”

Darasa: Maana ya msingi ya neno hili ni chumba ambamo mafunzo hutolewa shuleni. Kwa mfano, “Wanafunzi wamo darasani wanafunzwa na mwalimu.” Maana mpya ni kikundi cha wanafunzi wanaopata mafunzo pamoja. Kutokana na fasili hizi, tumebaini kuwa neno ‘darasa’ limetumiwa kumaanisha ‘kikundi cha wanafunzi.’ Kwa mfano, “Wanafunzi wengi hawapendi darasa la hesabu kwa kuwa linawapa matatizo.” Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa neno ‘darasa’ limechangia katika kuunda polisemi.

Dishi: Maana ya msingi ni sahani kubwa ya kupakulia chakula. Kwa mfano, “Mama alinunua dishi jana sokoni.” Maana mpya ni chakula. Kwa mfano,

“Juma na Maria walikula dishi ya wali wakamaliza.” Hapa tunaona kuwa leksimu ‘dishi’ imetumiwa kama metonimu ya ‘chakula’. Mhimili wa nadharia ya semantiki tambuzi unasisitiza kuwa binadamu ana umilisi mkubwa wa kuhusisha dhana zinazolandana kwa kutumia msingi wa maumbile. Ndiposa kutokana na maana mpya ya leksimu ‘dishi’ tunapata dhana kama vile, dishi ya nyama na dishi ya sima. Kwa hivyo, leksimu ‘dishi’ imechangia katika kuunda polisemi.

Fedha: Maana asilia ya leksimu hii ni madini yenye rangi kama ya bati. Kwa mfano, “Mimi ninazo pete za fedha, za dhahabu ni ghali nami sinazo.” Maana mpya ni pesa; fulusi. Kutokana na fasili hizo, tumebaini kuwa leksimu ‘fedha’ imetumika kama metonimu ya ‘pesa’. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa dhana pana (madini) imetumiwa kuwasilisha dhana finyu (pesa). Kwa mfano, “Bila ya kuwa na fedha mkononi hatuwezi kununua bidhaa sokoni.” Hali hii inaingiliana na mhimili wa nadharia ya semantiki tambuzi unaodai kuwa maana huwa na muundo wa kiensaiklopedia. Kwa hivyo, binadamu aliye na habari ya leksimu *fedha* pia hujua maelezo mengineyo yanayohusu fedha: yaani kazi yake na namna ambavyo zinaweza kupatikana. Kwa hivyo, leksimu ‘fedha’ imechangia katika uzuaji wa polisemi.

Ikulu: Maana ya msingi ya leksimu hii ni makao rasmi ya rais wa nchi. Kwa mfano, “Huko ikulu rais alipokea vitambulisho vya mabalozi watatu.” Maana mpya ni nyumba kubwa. Kwa mfano, “Yule bwana tajiri anaishi katika ikulu aliyojijengea yeye mwenyewe.” Kutokana na maelezo hayo, tumebaini kuwa

leksimu ‘ikulu’ imetumiwa kumaanisha ‘makao makuu ya rais’. Pia leksimu hiyo imechangia katika kuunda polisemi.

Jiko: Maana ya msingi ya neno hili ni mahali pa kupikia. Kwa mfano, “Mama yuko jiko anapika mboga.” Maana mpya ya neno hilo ni kifaa kinachotoa nishati ya kupikia. Kwa mfano, “Badala ya jiko la makaa baba ametununulia jiko la umeme.” Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa dhana pana (jengo ambamo mna jiko la kupikia chakula) imetumiwa kuwakilisha dhana finyu (kifaa kinachotoa nishati ya kupikia). Pia leksimu ‘jiko’ katika kamusi ni polisemi.

Jembe: Maana ya awali ya leksimu hii ni kifaa cha kulimia au kuchimbia ardhi chenye sehemu ya chuma bapa na mpini mrefu ambacho hushikwa mkononi. Kwa mfano, “Jembe la mzee kombo limevunjika mpini.” Maana ya awali ya leksimu hiyo imepanuka maana na kuwakilisha ‘mkulima’ yaani; mtu hodari wa kufanya jambo habagui zana ya kuitekelezea kazi hiyo. Kwa mfano, “mchagua jembe si mkulima” semantiki tambuzi hudai kuwa maana huwa na muundo wa kiensaiklopedia. Kwa hivyo, tumeona kuwa leksimu ‘jembe’ imepata maana mpya kutokana na maelezo mengineyo kuhusu leksimu hiyo, kama vile kazi yake.

Kiti: Maana ya msingi ya neno hili ni kifaa cha kukalia. Kwa mfano, “Kiti cha mwanafunzi yule kilivunjika jana.” Maana mpya ya neno *kiti* ni nafasi ya uongozi. Kwa mfano, “Kiti cha ugavana kinastahili kupewa mwananchi atakakayetuwakilisha vizuri.” Pia kutokana na maana ya ziada ya leksimu ‘kiti’ tunapata dhana mbalimbali kama vile ‘kiti cha seneti’, ‘kiti cha rais’ na ‘kiti cha

ubunge'. Maoni haya yanaingiliana na mhimili wa nadharia ya semantiki tambuzi unaodai kuwa maana imejikita katika maumbile ya binadamu yakiwa msingi wa kufasiri dhana ya ulimwengu. Kwa hivyo, ni wazi kuwa neno 'kiti' limetumiwa kama metonimu ya 'nafasi ya uongozi'. Vilevile neno hilo limechangia katika uzuaji wa polisemi.

Nyumba: Maana ya msingi ya leksimu hii ni jengo ambalo limekusudiwa kukaliwa na watu. Maana mpya ni mke; ahali. Fasili ya msingi ya leksimu hii imerejelea jengo wanamoishi watu; makao. Kwa mfano, "Nyumba yake haiko hapa, ipo mtaa wa pili." Kisha fasili ya pili imerejelea mke au familia. Kwa hivyo kutokana na fasili za leksimu 'nyumba' tumebaini kuwa leksimu 'nyumba' imetumiwa kwa maana ya 'familia' kwa mfano, "Leo ni miaka mitano tangu apate nyumba."

Mbele: Maana asilia za neno hili ni (1). kinyume na nyuma. (2). kabla ya wakati kuwadia. (3) mbele ya watu: hadharani. Kutokana na fasili hizo, ni wazi kuwa neno 'mbele' pia hutumika kuwakilisha wakati. Kwa mfano, "Mwanafunzi yule alifika kwenye shule mbele ya Mwalimu".

Mvi: Maana ya awali ya leksimu hii ni nywele nyeupe hasa za kichwani. Kwa mfano, "Babu amekuwa mzee sana na kichwa chote kimejaa mvi. Pia, leksimu hii hutumiwa kumaanisha 'uzee'. Kwa mfano, "Uzee wake ulijitokeza alipofikisha miaka hamsini. Kulingana na maelzo hayo, ni wazi kuwa leksimu 'mvi' hutumika kama metonimu ya uzee. Hali hii inlandana na mhimili wa semantiki unaodai kuwa maarifa ya kiutambuzi huwa katika kategoria zenye mizunguko. Leksimu ni kifaa kinachotumiwa na wasemaji katika kufikia ujuzi

uliyopo katika hifadhi ya maarifa katika utambuzi (Vyvyan na Greens,2006). Kile ambacho wanaeleza ni kwamba, leksimu inapotamkwa humchochea binadamu kufikia maana ya awali ya leksimu hiyo pamoja na mambo mengineyo yanayozunguka leksimu hiyo. Kwa mfano, maana ya msingi ya leksimu ‘mvi’ imetumiwa kuwakilisha dhana mpya ambayo ni ‘uzee’.

Taji: Maana asilia ya neno hili ni vazi la kichwani linalovaliwa na aghalabu mfalme au malkia. Kwa mfano, “Malkia wa Uingereza huvaa taji lake kila mwaka katika ufunguzi wa bunge la kitaifa.” Fasili mpya ya neno hili ni ubingwa aliopata mtu au timu katika michezo au mashindano. Kwa mfano, “Timu ya Kenya ilipata taji baada ya kucheza na timu ya Rwanda.” Kwa hivyo leksimu ‘taji’ imetumiwa kuwakilisha ‘ubingwa aliopata mtu au timu katika mashindano’. Kwa hivyo, neno ‘taji’ limechangia katika kuunda polisemi.

Kutokana na utafiti huu tumebaini kuwa polisemi zilizoundwa kutokana na metonimu vilevile huonyesha maana nyingi zenye etimolojia moja. Kwa hivyo, metonimu ni mfumo wa maana unaoangaza ndani; yaani neno au jina linalotumiwa kurejelea kitu kingine ambacho kinahusiana na hicho cha kwanza kwa namna fulani.

2.3 Hitimisho

Lengo la sura hii lilikuwa ni kubainisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu katika Kiswahili. Imebainika kuwa sitiari na metonimu huchangia pakubwa katika uzuaji wa polisemi katika Kiswahili. Pia imedhihirika kwamba maana za sitiari na metonimu huweza kuhamishwa na kutumika katika nyanja nyingine ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Hali hii

huwepo kwa sababu kuna sifa fulani za kimsingi za kufanana katika vitajwa viwili.

SURA YA TATU

UAINISHAJI WA POLISEMI

3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu kwa lengo la kuziainisha. Katika kuziainisha polisemi hizo, tulitumia uainishaji wa kiutambuzi, kiuamilifu, kijiografia, kitabia na kiuhusiano. Uainishaji wa kiutambuzi ulihusisha polisemi za viumbe hai kama vile wanyama na binadamu. Uainishaji wa kiuamilifu nao ulihusisha polisemi za utendakazi wa kitu na chombojikoni.

Uainishaji wa kijiografia ulijumuisha polisemi za mahali kama vile makao. Uainishaji wa polisemi kwa mtazamo wa kitabia vilevile ulihusisha polisemi za viumbe hai kama vile wanyama na binadamu. Mwisho, uainishaji wa kiuhusiano ulihusisha polisemi za wadudu, wanyama, sehemu za mwili wa binadamu na kadhalika.

Katika semantiki tambuzi, polisemi huchukuliwa kama iliyoundwa na watu au vitu vya familia moja vyenye sifa zinazofanana. (Sun, 2019). Kwa hivyo, huchukua mtazamo wa kiuainishi ambapo vitu vyenye sifa sawa huwekwa pamoja. Katika hali hii kutawepo na maana ya kimsingi iliyo rahisi kueleweka. Maana hii ya kimsingi itawezesha kueleweka kwa maana hizo zingine ambazo zimezalishwa kisitiari au kimetonimu. Kwa hivyo, data ya utafiti huu imeainishwa kwa msingi mkuu wa semantiki tambuzi ambao ni uainishaji.

3.1 Uainishaji wa polisemi za Kiswahili

Katika kugawa data kuhusu polisemi katika Kiswahili tulizingatia vigezo vifuatavyo; utambuzi, uamilifu, mtazamo wa kitabia, uhusiano na mahali.

3.2 Uainishaji wa polisemi kiutambuzi

Katika kumbo hili, tumebaini kuwa data nyingi ya utafiti huu ilikuwa na mwelekeo wa kiutambuzi. Uainishaji kiutambuzi hutumiwa kutambua vitu kwa mujibu wa jinsi vitu vinavyofanana na namna vinavyoonekana. Uainishaji wa aina hii hutumiwa kuchunguza umbo la kitu fulani na kurejelea kufanana kwake na kitu kingine ili kuunda uwanda mmoja maalumu wa kileksika na kisemantiki (Okal, 2018). Katika kumbo hili tulipata aina ya polisemi ifuatayo;

Polisemi za sehemu za mwili

Pia data ya utafiti huu ilijumuisha polisemi zinazorejelea viungo au sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu. Kwa mfano, *mkono*, *jicho*, *jino*, *ulimi* na *mguu*. Kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)*, leksimu *mkono* ina maana nne ambazo ni; (i) kiungo cha binadamu kilichounganishwa kwenye bega kinachotumiwa kushika vitu. (ii) kifaa chochote kinachotumiwa na au kufanya kazi ya kushikia vitu (iii) sehemu ndogo ya kitu inayojiunga au kutoka kwenye kitu hicho; dhiraa. Neno *jicho* lina maana tatu kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)* ambazo ni; (i) kiungo cha mwili cha kuonea. (ii) panda liwekwalo katika gubeti ya jahazi. (iii) chipukizi la ua. Leksimu *jino* ina maana tatu ambazo ni: (i) kipande kigumu cheupe kilicho kinywani mwa binadamu au mnyama kinachotumiwa kutafunia chakula au kukata vitu (ii) kifaa

kinachotekeleza kazi kama jino la binadamu kinachotumika kukatia, kutafunia au kushikilia vitu vingine (iii) ugonjwa wa meno au ufizi.

Leksimu *ulimi* ina maana tatu katika kamusi ambazo ni; (i) Kiungo cha mwili ndani ya kinywa kinachotumika kuonjea, kusemea, kurambia, na kadhalika (ii) Kitu chochote kinachofanana na ulimi (iii) shungi la miali ya moto hasa inapoonekana kwa umbali. Maana ya msingi ya neno *mguu* ni kiungo cha mwili wa binadamu, mnayama au mdudu kinachomwezesha kusimama au kwenda. Maana mpya ni kitu chochote kinachofanya kazi kama hiyo.

Tukichunguza kwa makini mifano ya polisemi za sehemu za mwili, tutabaini waziwazi kuwa maana ya msingi ya leksimu ‘mkono’, ‘jicho’, ‘jino’, na ‘ulimi’ imehamishwa kisitiari na kuhusishwa katika vitu vingine. Kwa mfano, kutokana na umbo la *mguu* wa binadamu kufanana kwake na kitu kingine chenye uwezo wa kutenda kama *mguu*, tunapata dhana kama vile, “*mguu wa kiti*” na “*mguu wa meza*”. Pia tuliona kuwa leksimu ‘jicho’, ‘mkono’, ‘jino’, na ‘ulimi’ zimehusishwa na kutumika na vitu vingine kutokana na jinsi vinavyofanana kiumbo. Kwa mfano, leksimu ‘jicho’ huhusishwa na vitu vingine kama vile, ‘jicho la viazi’, ‘jicho la sindano’ na ‘jicho la muhogo’. Leksimu ‘mkono’ huhusishwa katika vitu vingine kama vile mkono wa shati na mkono wa birika. Pia moto unapowaka kwa kuchomozachomoza juu, umbo lake hufanana na ulimi wa binadamu. Kutokana na maelezo hayo tunapata dhana kama vile ‘ulimi wa moto’. Wanasemantiki tambuzi hueleza kuwa maana imejikita katika maumbile ya binadamu yakiwa msingi wa kufasiri dhana zingine katika ulimwengu wake. Maumbile na umbo lake binadamu

humwezesha kufasiri ishara mbalimbali katika ulimwengu wake, kile wanasemantiki tambuzi huita picha.

3.3 Uainishaji wa polisemi kwa mtazamo wa kitabia

Katika uainishaji huu, tulijikita tu katika viumbe hai. Kwa mujibu wa Mdee na wenzie (2011), kiumbe hai ni kitu chenye uhai kwa mfano, binadamu, ndege, wadudu na kadhalika. Katika kumbo hili tulibainisha leksimu zifuatazo; *fisi*, *chui*, *beberu*, *gwagu*, *kinyonga*, *sungura*, *kupe*, *kasuku* na *chiriku*. Kisha tukaziainisha leksimu hizo katika makundi mbalimbali kama ilivyo hapa chini.

3.3.1 Polisemi za wanyama

Kutokana na leksimu za kumbo hili, tulibaini kuwa leksimu hizo zinazohusu aina mbalimbali za wanyama pori na wanyama wa nyumbani. Kwa mfano, *fisi*, *chui*, *beberu*, *gwagu*, *kinyonga* na *sungura*. Maana ya msingi ya leksimu *fisi* ni mnyama wa mwituni mwenye ukubwa kama *beberu*, aliye na rangi ya kijivu na anayeaminiwa kuwa ni mwoga na anayependa sana kula mizoga. Maana mpya ni mtu mlafi. Kwa mfano, “Maria ni *fisi* karamuni.” Kauli hii inamaanisha kuwa Maria ni mlafi akiwa karamuni. Maana ya msingi ya neno *chui* ni mnyama kama paka lakini mkubwa. Maana ya pili ni mtu mkali. Kwa mfano, “Riziki ni **chui** nyumbani”. Kauli hii inamaanisha kuwa Riziki ni mtu mkali hasa akiwa nyumbani. Katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)*, maana za leksimu *beberu* zimeorodheshwa zikiwa tano; (a) mbuzi dume (b) mwanamume mwenye nguvu (c) mtu anayetoa harufu mbaya (d) Taifa linalotawala nchi nyingine kiuchumi au kisiasa (e) mtu anayeamini na kutekeleza siasa ya ubeberu. Kwa mfano, “Amani ni **beberu** shuleni.” Kauli

hii inamaanisha kuwa Amani ni mtu anayeeneza siasa ya ubeberu akiwa shuleni ama pia inaweza kumaanisha mtu mwenye nguvu hasa akiwa shuleni. Maana ya awali ya neno *gwagu* ni paka aliyeasi na kukimbilia porini. Maana mpya ni mtu mwovu. Kwa mfano, “Christine ni gwagu klabuni.” Kauli hii inamaanisha kuwa Christine ni mtu mbaya akiwa klabuni.

Maana asilia ya neno *kinyonga* ni mnyama mdogo anayebadilika rangi ya mwili wake ili ifanane na rangi ya mazingira alimo na maana mpya ni mtu wa kubadilikabadilika; kigeugeu. Kwa mfano, “Musa ni **kinyonga** kazini.” Kwa upande mwingine, maana ya msingi ya leksimu ‘sungura’ ni aina ya mnyama mdogo kama paka ambaye miguu yake ya nyuma ni mirefu kuliko ya mbele, mwenye mkia mfupi na masikio marefu, ambaye huchimbua ardhi, hula majani na huenda kasi kwa kurukaruka. Maana mpya ni mtu mjanja na mwerevu. Kwa mfano, sentensi “Juma ni **sungura** shuleni.” ina maana kuwa Juma ni mtu mjanja akiwa shuleni. Katika mifano ya hapo juu, tumeona kuwa polisemi zilizokolezwa rangi zinahusu majina ya wanyama. Majina hayo yote yanawakilisha viumbe wanaopatikana katika ulimwengu halisi. Pia katika mifano hiyo hiyo, tulibaini kuwa ingawa polisemi zilizokolezwa rangi ni majina ya wanyama lakini kwa upande mwingine yametumika kuwakilisha dhana zinazohusu binadamu.

Sentensi, “Maria ni fisi karamuni” ina maana kuwa Maria ni mtu mlafi akiwa karamuni. Katika jamii nyingi, fisi husemekena kuwa ni mnyama ambaye hatosheki na kitu kimoja; yaani ni mnyama ambaye ana tamaa. Kwa hali kama hiyo mtu yeyote ambaye anaonekana kuwa na tabia za ulafi huitwa fisi. Kwa

hivyo, hapa tunaona kwamba Maria amefananishwa na *fisi* kulingana na tabia yake inayofanana na ya *fisi*. Katika mfano mwingine sentensi, “Riziki ni chui nyumbani” ina maana kuwa Riziki ni mtu mkali akiwa nyumbani. Katika jamii ya wanyama, chui ni mnyama anayeogopwa na wanyama wengine kama vile swara, na pia kwa wanadamu, chui ni mnyama anayeogopwa sana kutokana na ukali wake. Kwa hivyo, Riziki hapa amefananishwa na chui kutokana na tabia zake za ukali. Katika mfano mwingine, sentensi “Amani ni beberu shuleni”, inamhusisha Amani na beberu kutokana na tabia zake zinazolandana na zile za beberu. Katika mfano huu wa sentensi “Rose ni gwagu klabuni”, Rose amehusishwa na gwagu kutokana na tabia zake ambazo zinafanana na za mnyama huyo.

Kutokana na maelezo hayo, tumeona kuwa polisemi za wanyama ambazo zimebainishwa katika kundi hili ni maneno ya kikoa kimoja, yote yanaonyesha namna fulani ya uhusiano wa kitabia unaojitokeza baina ya watu na wanyama. Pia tumebaini kwamba katika polisemi hizo za wanyama, dhana zake zote zinapatikana katika maana mpya (ambazo zimehusishwa na watu). Kusema kweli zimetokana na mazoea ya kimazingira na utamaduni wa watu wenyewe. Nadharia ya semantiki tambuzi husisitiza kuwa binadamu ana tajiriba kubwa ya kuhamisha dhana toka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine katika mawanda ya kiutambuzi. Katika mifano ya polisemi za hapo juu, tabia ya wanyama na wadudu imehamishwa na kuihusisha na tabia ya binadamu. Kwa mfano, sentensi, “Riziki ni chui nyumbani” tumeona kuwa ‘Riziki’amefungwa kwa ‘chui’ na kwa kuwa tanafahamu kwamba chui ni

mkali, kupitia kwa chui, sifa ya ukali inahamishwa hadi kwa Riziki; sifa ambayo si yake kwa desturi.

3.3.2 Polisemi za wadudu

Katika kundi hili tuliweza kubainisha mfano mmoja kulingana na data ya utafiti wetu. Maana ya awali ya neno ‘kupe’ ni mdudu ambaye hung’ang’ania kwenye miili ya wanyama na kuwafyonza damu. Maana ya pili ni mtu anayepata mapato bila ya kutumia jasho lake. Kwa mfano, “Ali ni *kupe* nyumbani.” Katika kauli “Ali ni *kupe* nyumbani”, Ali amefananishwa na kupe. Hii ni kwa sababu Ali hashughuliki ili kupata riziki kujikimu yeye mwenyewe, hutegemea kupata chakula na mahitaji yake kutokana na jasho la watu wengine. Hii kwa hakika ndiyo tabia aliyo nayo kupe ya kufyonza na kunyonya damu za viumbe wengine.

3.3.3 Polisemi za ndege

Kutokana na data ya utafiti huu, tumebaini kuwa ilikwa na polisemi za majina ya ndege. Kwa mfano, *kasuku* na *chiriku*. Maana ya kamusi za neno ‘kasuku’ ni ndege mkubwa mwenye rangi nyingi anayeweza kuiga kusema kama binadamu na mara nyingi hufugwa majumbani. Maana mpya ni mtu mwenye tabia ya kusema maneno mengi aghalabu kwa kuiga bila umakini. Kwa mfano, “Kazija ni kasuku nyumbani.” Katika sentensi hii, Kazija amepewa jina la kasuku kutokana na tabia zake za kusema maneno mengi aghalabu kwa kuiga. Jina lingine la ndege ambalo ni polisemi ni chiriku. Maana ya msingi ya leksimu ‘chiriku’ ni ndege mdogo mwenye kelele sana. Maana ya pili ni mtu apendaye kusemasema. Kwa mfano, “Rehema ni chiriku sokoni.” Hii ni

kutokana na sifa zake ambazo zinafanana na zile za chiriku. Kwa hali kama hiyo mtu yeyote ambaye anaonekana kuwa na tabia ua kusemasema maneno bila kuzingatia kile anachosema huitwa chiriku.

Tukichunguza kwa makini maelezo ya hapo juu tutabaini kuwa polisemi zilizotolewa katika kundi hili pia ni polisemi za kikoa kimoja, zote zinaonyesha namna fulani ya uhusiano wa kitabia unaojitokeza baina ya ndege na binadamu. Pia nadharia ya semantiki tambuzi hufafanua kuwa maana hujikita katika utamaduni na tajriba za pamoja za wanajamii. Ni katika huu msingi ambapo jamii huelekea kuwatazama viumbe hawa kwa namna ya kipekee kidogo. Kila kiumbe huhusishwa na sifa fulani kutokana na tabia yake. Vilevile, jamii nyingi za kiafrika, ambako viumbe hawa pia hupatikana, huwatazama viumbe hawa kwa namna hiyo hiyo.

3.4 Uainishaji wa kiuamilifu

Uainishaji huu huweza kurejelea sio tu kazi za vifaa bali pia sehemu mbalimbali za vitu au za binadamu. Kutokana na data ya utafiti wetu, tumeweza kubainisha polisemi za majina ya sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu na majina ya vifaa ambavyo hutumiwa jikoni. Kwa mfano, mkono, mguu, jiko na dishi. Polisemi hizo tumeziainisha kama ifuatavyo:

3.4.1 Polisemi zinazorejelea utendakazi wa kitu

Katika kundi hili, data ambayo ilichanganuliwa ni *mguu* na *mkono*. Maana ya msingi ya leksimu ‘mguu’ ni kiungo cha mwili wa binadamu, mnyama au mdudu kinachomwezesha kusimama au kwenda. Kwa mfano, “Hakuna mtu anayeweza kutembea kwa *mguu* mmoja.” Maana mpya ya leksimu ‘mguu’ ni

kitu chochote kinachofanya kazi kama mguu. Leksimu *mkono* ina maana nne katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)* ambazo ni; (i) kiungo cha mtu kilichounganishwa kwenye bega kinachotumiwa kushika vitu. (ii) kitu chochote kinachotumiwa na au kufanya kazi ya kushikia vitu (iii) sehemu ndogo ya kitu inayojiunga au kutoka kwenye kitu hicho; dhiraa. Tukichunguza kwa makini maana mpya za leksimu *mguu*, na *mkono* ni wazi kuwa maana hizo zimerejelea kazi ambayo sehemu hizo hutekeleza katika mwili wa binadamu. Nadharia ya semantiki tambuzi inaeleza kuwa binadamu ana uwezo mkubwa wa kuainisha vitu mbalimbali ambapo vitu vyenye sifa sawa huwekwa pamoja. Katika kundi hili, tumebainisha leksimu ‘mguu’ na ‘mkono’ kama polisemi zinazorejelea utendakazi wa kitu. Kwa mfano, kazi mojawapo ya mkono ni kushika.

3.4.2 Polisemi za chombojikoni

Chombojikoni hurejelea vifaa ambavyo hutumiwa jikoni (Okal, 2018). Chombojikoni ni neno ambalo limeundwa kutokana na mwambatanisho ambapo maneno mawili huambatishwa ili kuunda neno moja. Kwa hivyo, chombojikoni limeundwa kutokana na kuambatisha neno ‘chombo’ na ‘jikoni’ kuunda chombojikoni. Kutokana na maelezo hayo, tunaweza kusema kuwa polisemi za chombojikoni hurejelea vifaa ambavyo hutumiwa jikoni kutekeleza kazi mbalimbali. Katika kundi hili tulibainisha polisemi mbili pekee kulingana na data yetu ya utafiti. Data ambayo ilichanganuliwa ni *jiko* na *dishi*. Maana ya msingi ya neno *jiko* ni mahali pa kupikia. Kwa mfano, “Mama yuko jiko anapika mboga.” Kwa upande mwingine maana mpya ya neno ‘jiko’ ni kifaa

kinachotoa nishati ya kupikia. Kwa mfano, “Badala ya jiko la makaa baba ametununulia jiko la umeme.”

Maana ya msingi ya neno ‘dishi’ ni sahani kubwa ya kupakulia chakula. Kwa mfano, “Mama alinunua dishi jana sokoni.” Maana mpya ni chakula. Kwa mfano, “Juma na Maria walikula dishi ya wali wakamaliza.” Tukichunguza mifano katika kundi hili ni wazi kuwa ni vyombo ambavyo hutumika kutekeleza kazi maalum hasa jikoni. Nadharia ya semantiki tambuzi hufafanua kuwa maana huwa na muundo wa kiensaiklopedia. Kutokana na mhimili huu ni wazi kuwa anayejua maana ya msingi ya leksimu fulani pia hujua maana zingine za leksimu hiyo, yaani mahali leksimu hiyo hupatikana na kazi yake mahususi.

3.5 Uainishaji wa Kijiografia

Kutokana data ya utafiti wetu, tumebaini kuwa ilikuwa na polisemi za majina ya mahali. Kwa mfano, Ikulu, Darasa, choo na jiko. Maana ya awali ya leksimu ‘Ikulu’ ni makao rasmi ya rais wa nchi. Kwa upande mwingine, maana mpya ni nyumba kubwa. Kwa hivyo, leksimu ‘ikulu’ hutumiwa kuwakilisha ‘makao ya rais’.

3.6. Uainishaji wa polisemi kihusiano

Uainishaji huu unahusu namna maana za leksimu zinavyohusiana. Katika kumbo hili, tuliainisha aina za polisemi zifuatazo; polisemi zenye uhusiano wa ki-mahali, polisemi zenye uhusiano wa sifa na polisemi zenye uhusiano wa kiumbo kisha tumezjadili moja baada ya nyingine kama ifuatavyo;

3.6.1 Polisemi zenye uhusiano wa ki-mahali

Hizi ni polisemi ambazo huhusisha dhana ya mahali. Tuzingatie mifano ifuatayo;

Jedwali 3.1: Polisemi zenye uhusiano wa ki-mahali

<i>Leksimu</i>	<i>Maana ya asilia</i>	<i>Maana ya ziada</i>
Mguu	Kiungo cha mwili wa binadamu, mnyama au mdudu kinachomwezesha kusimama au kwenda.	Kitu chochote kinachofanya kazi kama mguu.
Jino	Kipande kigumu cheupe chenye enemeli kilichopo kwenye taya za wanyama kinachotumiwa kutafunia chakula au kukata vitu.	Kitu au kifaa kinachofanya kazi kama jino la wanyama kukatia na kutafunia vitu vingine.
Shingo	Sehemu ya mwili inyounganisha kichwa na sehemu zingine za mwili.	Ni sehemu yoyote nyembamba ya chupa inayounganisha mdomo wa chupa na sehemu yake nyingine.
Mlango	Uwazi au nafasi maalumu iliyo ukutani ili kuingilia na kutokea mahali penye uwazi zaidi.	Kizuizi kilichotengenezwa kwa ubao, chuma au kitu kingine chochote ili kuziba uwazi wa kuingilia na kutokea kwenye ukuta au kiambaza cha jengo, chumba au gari.
Tako	Ni sehemu ya nyuma ya mwili wa binadamu baina ya kiuno na paja inayotumika kukalia.	Ni sehemu ya chini ya kitu au kifaa ambacho hutumiwa aghalabu kuwa kikalio.
Lango	Eneo lililo katikati ya nguzo mbili katika pande mbili zinazotazamana na uwanja ambapo sharti mpira uingie ili kuhesabu goli au bao.	Ni mlango mkubwa unaotumika kuingilia ndani ya uwanja, mji, ngome na kadhalika.

Hapa tulibaini kuwa sifa ya mahali fulani inahamishwa na kuhusishwa na nyingine inayolandana nayo na kuzua leksimu mpya yenye maana tofauti. Kwa mfano, leksimu ‘mguu’ maana yake ya asilia imehusishwa na kitu chochote kinachofanya kazi kama mguu wa binadamu. Kutokana na fasili hii tunapata leksimu mpya kwa mfano, “mguu wa meza”. Pia katika leksimu ‘jino’ tulibaini kuwa leksimu hiyo imehusishwa na nyingine na kurejelea kitu kinachofanya kazi kama jino la mtu kinachotumika kukatia. Kutokana na maelezo hayo tunapata leksimu mpya ambayo ni “jino la msumeno”.

Pia, leksimu ‘shingo’ ambayo maana yake asilia ni sehemu ya mwili inayounganisha kichwa na sehemu zingine za mwili wa binadamu. Maana hii imepanuka kisitiari na kurejelea sehemu yoyote nyembamba ya chupa inayounganisha mdomo wa chupa na sehemu yake nyingine. Kwa hivyo ni wazi kuwa maana ya asilia ya leksimu ‘shingo’ imehamishwa na kuhusishwa na maana nyingine inayolandana nayo na kuzua leksimu mpya ambayo ni “shingo ya chupa”. Kwa hivyo, kutokana na maelezo hayo, tumebaini kuwa data ambazo zimechanganuliwa katika kundi hili, zote zimehusishwa na dhana ya mahali ambapo sifa ya mahali inahamishwa na kuhusishwa na nyingine inayohusiana nayo ili kuzua leksimu mpya.

3.6.2 Polisemi zenye uhusiano wa sifa

Hizi ni polisemi ambazo uhusiano wake unatokana na kitu kimoja na kingine kwa misingi ya tabia au sifa zilizopo baina ya dhana hizo mbili. Pia, sifa ya dhana ya ziada hutokana na dhana ya msingi. Tuchunguze mifano ya polisemi zifuatazo;

Jedwali 3.2: Polisemi zenye uhusiano wa sifa

<i>Leksimu</i>	<i>Maana ya msingi</i>	<i>Maana ya ziada</i>	<i>sifa inayofanana</i>
Ndumaku -wili	Kiumbe afananaye na nyoka husemwa kuwa ana vichwa viwili.	Mtu ajifanyaye mwema na rafiki, kumbe yu mwovu.	Sifa ya kutokuwa na msimamo.
Chiriku	Ndege mdogo mwenye kelele.	Mtu apendaye kusemasema	Kupiga kelele
Kupe	Mdudu ambaye hung'ang'ania kwenye miili ya wanyama na kuwafyonza damu.	Mtu anayepata mapato au matunda bila ya kutumia jasho lake.	sifa ya utegemezi.
Firauni	Jina la cheo cha wafalme wa zamani wa Misri.	Mtu yeyote mwenye vitendo vichafu.	Sifa ya kuwatesa wenziwe.

Nadharia ya semantiki tambuzi hufafanua kuwa binadamu ana ujuzi wa kuhamisha kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine katika mawanda ya kiutambuzi. Kinachohamishwa huwa hulka, picha ya umbo au utendakazi wa kitu kwa kuihusisha na hulka au umbo au utendakazi wa kitu kingine. Kwenye Jedwali 3.2, tulibaini kuwa maana za msingi za leksimu zimepanuka kisitiari na kuzua maana ya ziada. Pia, maana za ziada zilihusishwa na maana za msingi kutokana na uhusiano uliopo wa sifa baina ya maana hizo. Kwa mfano, maana ya kimsingi ya leksimu 'ndumakuwili' ni kiumbe afananaye na nyoka anayesemekana kuwa na vichwa viwili ambaye huuma kila upande. Kwa hivyo, kutokana na fasiri hizo tumeona kuwa sifa ya kutokuwa na msimamo imejitokeza kutokana na sifa ya ndumakuwili ya kuuma kila upande.

Aidha, leksimu ‘chiriku’ ambayo maana yake ya awali ni ndege mdogo mwenye kupiga kelele kila mara. Maana hii imepanuka kisitiari na kupata maana ya ziada ambayo ni mtu anayependa kusemasema maneno. Kutokana na fasiri hizo, tulibaini kuwa uhusiano wa sifa unaojitokeza hapa ni wa kupiga kelele. Pia kwenye Jedwali 3.2 ilibainika kuwa maana za msingi za leksimu *ndumakuwili*, *chiriku*, *kupe*, na *firauni* zinahusiana moja kwa moja na maana za ziada za leksimu hizo.

3.6.3 Polisemi zenye uhusiano wa Kiumbo

Hizi ni polisemi ambazo uhusiano wake unatokana na kuhusishwa umbo au umbile halisi au la kufikirika tu la dhana X na dhana Y. Vyavyan na Greens (2006) na Lemmens (2017) wanaeleza kuwa maumbile na umbo lake binadamu humjengea binadamu misingi ya kufahamu dhana mbalimbali katika mazingira yake, kile wanasemantiki tambuzi huiita picha au taswira. Hebu tuzingatie mifano katika jedwali lililo hapa chini.

Jedwali 3.3: Polisemi zenye uhusiano wa kiumbo

Leksimu	Maana ya msingi (x)	Maana mpya (y)	Uhusiano (x-y)
Nyundo	Kifaa kinachotumika kugongomelea katika shughuli za ujenzi kama vile useremala au ufundi.	Mtu mfupi.	Umbo la maumbile.
Nyonyo	Ni ncha ya titi.	Mpira mfano wa chuchu anaobembeleza mtoto au unaotiwa maziwa kwa ajili ya mtoto kunyonya.	Umbo la maumbile.
Mzinga	Kitu kirefu aghalabu cha mviringo chenye uwazi ndani kinachotengenezwa kwa mbao au mti.	Chombo kinachotengenezwa kwa chuma chenye mwanzi mkubwa ambao hutumika kurushia risasi kwa nguvu zaidi au mbali zaidi kuliko bunduki.	Umbo la mviringo
Mlango	Uwazi au nafasi maalumu iliyo ukutani ili kuingilia na kutokea mahali penye uwazi zaidi.	Kizuizi kilichotengenezwa kwa ubao, chuma au kitu kingine chochote ili kuziba uwazi wa kuingilia na kutokea kwenye ukuta au kiambaza cha jengo, chumba au gari	Kuwepo kwa uwazi
Lango	Eneo lililo katikati ya nguzo mbili katika pande mbili zinazotazamana na uwanja ambapo sharti mpira uingie ili kuhesabu goli au bao	Mlango mkubwa unaotumika kuingilia ndani ya uwanja, mji, ngome na kadhalika.	Kuwepo kwa uwazi.

Katika Jedwali 3.3 tumebaini kuwa maana za leksimu katika Y zina uhusiano wake katika X. Kwa mfano, leksimu 'nyundo' (kifaa kinachotumika

kugongomelea katika shughuli za ujenzi kama vile useremala au ufundi) ina uhusiano wa kiumbo (Ufupi) na leksimu ‘nyundo’ (Mtu mfupi). Aidha, leksimu *nyonyo* (Ncha ya titi) ina uhusiano wa kimaumbile na leksimu ‘nyonyo’ (Mpira mfano wa chuchu anaobembelezewa mtoto mchanga asilie au unaotiwa maziwa kwa ajili ya mtoto kunyonya). Pia leksimu ‘mzinga’ (Kitu kirefu angalau cha mvingo chenye uwazi ndani kinachotengenezwa kwa mbao au mti) ina uhusiano wa kiumbo na leksimu ‘mzinga’ (Chombo kinachotengenezwa kwa chuma chenye mwanzi mkubwa ambao hutumika kurushia risasi kwa nguvu zaidi na mbali zaidi kuliko bunduki. Pia, kwenye jedwali hilo, leksimu ‘lango’ (Eneo lililo katikati ya nguzo mbili katika pande mbili zinazotazamana na uwanja ambapo sharti mpira uingie ili kuhesabu goli au bao) ina uhusiano wa kuwepo kwa uwazi na leksimu ‘lango’ (Mlango mkubwa unaotumika kuingilia ndani ya uwanja, mji na ngome.) Kutokana na maelezo hayo, tumebaini kuwa umbo X ndio msingi wa uhusiano wa umbo Y. Pia, nadharia ya semantiki tambuzi hueleza kuwa binadamu ana uwezo wa kipekee wa kuhamisha dhana fulani kutoka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine katika mawanda ya kiutambuzi. Kwa hivyo, hapa ni dhahiri kuwa kilichohamishwa ni umbo.

3.7 Hitimisho

Sura ya tatu imejadili uainishaji wa polisemia katika Kiswahili. Tumebainisha kuwa baadhi ya polisemi ziligawika katika zaidi ya kundi moja. Kwa mfano, katika uainishaji wa polisemi za kiutambuzi, leksimu ‘mkono’ iliainishwa kama polisemi ya sehemu ya mwili. Vilevile leksimu hiyo iliainishwa katika uainishaji wa kiuamilifu kama polisemi zinazorejelea utendakazi wa kitu. Pia,

ilibainika kuwa maana ya msingi na maana ya ziada za leksimu huwa na uhusiano wa namna fulani. Hii ilijitokeza hasa katika polisemi zenye uhusiano mbalimbali. Polisemi zilizobainishwa kutokana na vigezo mbalimbali ni; polisemi za wanyama, polisemi za sehemu za mwili, polisemi za wadudu, polisemi zenye uhusiano wa kimatumizi, polisemi zenye uhusiano wa kitabia na polisemi zenye uhusiano wa kiumbo.

SURA YA NNE

MCHAKATO AMBAO SITIARI NA METONIMU HUPITIA KUUNDA

POLISEMI

4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia kuunda polisemi katika Kiswahili. Mchakato ni mfululizo wa shughuli unaosababisha kitu fulani kufanyika au lengo fulani kufikiwa (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2018). Kama ilivyoielezwa katika sura zilizotangulia, polisemi ni neno au kishazi chenye maana mbalimbali zinazohusiana. Sun (2019) anasema kuwa karibu maneno yote ya lugha ni ya kipolisemi kwa sababu maneno huwa na maana ya kimsingi na maana nyingine isiyo ya moja kwa moja. Maana hii ya pili hutokana hasa na matumizi ya neno hilo katika muktadha mahususi. Suala la kutenganisha maana ya kimsingi na maana husishi limeshughulikiwa katika fahiwa za sitiari na metonimia. Maana hii ya kimsingi hutuwezesha kuelewa maana hizo zingine zilizohusishwa nayo. Kutokana na kuasisiwa kwa isimu tambuzi katika miaka ya 1980 kulileta njia mpya ya kuchunguzia polisemi. Wanaisimu tambuzi huweka umuhimu mkubwa kwa dhima ya maana, michakato dhanifu na tajriba katika uchunguzi wa lugha na akili ya binadamu na jinsi vitu hivi vinaingiliana. Vipashio hivi huingiliana katika mfumo wa kisemantiki unaoitwa mtandao dhanifu.

4.1 Mchakato ambao sitiari hupitia kuunda Polisemi

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo inalinganisha vitu au watu lakini bila kutumia viunganishi (Chacha na Pendo, 2019). Katika sitiari, kuna uhamishaji wa maana na hisi kutoka kitu kimoja hadi kitu au dhana nyingine tofauti. Vitu

hivyo viwili vinavyohusishwa kwa kawaida huwa havina uhusiano wa moja kwa moja. Kwa mfano, unaposema “Maria ni chui” ukimaanisha kuwa Maria ni mkali, yaani ana ukali wa kudhalilisha. Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema kuwa sitiari huwa na sehemu tatu: kizungumzwa, kiungo na kifananishi. Katika mfano wa “Maria ni chui”, kizungumzwa ni Maria, kifananishi ni chui na kiungo ni ukali.

Kizungumzwa - Kiungo - Kifananishi

Maria - Ukali - Chui

Katika nadharia ya Isimu Tambuzi, sitiari dhanifu hurejelea uelewa wa wazo moja, au kikoa dhana, kwa mujibu wa kingine. Katika muktadha huu, sitiari dhanifu au ya kimawazo hutoa aina mbili za maeneo ya ufahamu; moja ni ile inayotokana na mambo tunayoyaona (Maria, chui) na nyingine ni ile ya kidhahania (ukali). Hiyo ya kwanza inaitwa eneo chasili/chanzo na ya pili inaitwa eneo lengwa. Eneo chanzo hutumiwa ili kuwezesha eneo lengwa kueleweka. Hali hiyo inaweza kuwasilishwa kwa njia ya kielelezo kama ifuatavyo:


maumbo ya kidhahania (eneo lengwa)



maumbo tunayoyaona (eneo chasili)


Kwa hiyo, sitiari “Maria ni chui” ina maumbo mawili: Maria na chui, ambayo ni yale tunayoyaona kwa upande mwingine kuna maumbo ya kidhahania (ukali) yale tusingiyoona. Sitiari dhanifu hutuletea kipengele cha maumbo ya

kidhahania ambayo yanalinganishwa na maumbo yanayoonekana ijapokuwa si kwa njia ya moja kwa moja. Matokeo yake yanaoneshwa katika mchoro huu:




Mchoro 4.1: Maumbo ya kidhahania

Katika sitiari “Maria ni chui”, tunajua kwamba chui anayo sifa ya ukali. Ili Maria aweze kuwa chui basi itahitajika kwamba yeye pia awe na sifa za ukali. Hicho ndicho kitu cha kidhahania kinachounganisha Maria na chui. Sitiari hizi za kimawazo hutuwezesha kutumia maneno kutoka eneo moja (Maria/chui) kuzungumzia maneno ya eneo lingine (Ukali). Kwa mujibu wa sehemu za sitiari kama walivyopendekeza Mulokozi na Kahigi (1979), mchakato utakuwa:



Matumizi haya mapya ya neno ‘chui’ yanapoendelea kwa muda mrefu yanazua polisemi ambapo neno ‘chui’ kwa sasa lina maana ya: 1. mnyama anayekula nyama ambaye anafanana na paka mkubwa na mwenye kasi sana na hupatikana Asia na Afrika 2. mtu mwenye ukali mwingi hasa wenye kudhalilisha (*Kamusi ya Karne ya 21*). Ifahamike kwamba wakati maneno yanapata maana mpya kupitia kwa matumizi, maana za zamani hubaki katika lugha. Kwa hiyo,

polisemi inahusu uwepo sambamba wa maana mpya na maana ya zamani. Polisemia huzuka kwa kulifunga neno linalofahamika ‘kimkufu’ kwa neno lisilofahamika. Katika mfano wa hapo juu, ‘Maria’ anafungwa kwa ‘chui’, na kwa kuwa tunajua kwamba chui ni mkali, kupitia kwa chui, sifa ya ukali inahamishwa hadi kwa Maria; sifa ambayo si yake kwa desturi. Hii ni njia moja ya upanuzi wa maana katika semantiki. Hali hiyo inaweza kuwasilishwa kimchoro ifuatavyo:



Mchoro 4.2: Kufananisha

Mchoro huu wa hapo juu unaonesha kuwa katika kiwango cha chanzo, Maria analinganishwa na chui lakini kisitiari chui anayo sifa ya ukali. Kwa kuwa ni muhali kumlinganisha binadamu na mnyama, ni wazi kuwa kinacholinganishwa ni sifa aliyo nayo chui ambayo ni ukali. Kutokana na ukali


wa chui tunapata kuwa katika mlinganisho huo lazima Maria awe mkali pia. Hivyo ndivyo neno ‘chui’ linavyopata maana ya pili ya ‘mtu mwenye ukali mwingi hasa wenye kudhalilisha kwenye kamusi na hivyo kuwa polisemi.

Maneno yanapopata maana mpya kupitia kwa matumizi, hasa ya kisitari, maana ya awali inaendelea kutumiwa. Kwa hiyo, polisemi huhusisha matumizi sambamba ya maana ya zamani na maana mpya kutokana na maana mpya kuzoeleka. Mchoro unaofuata unaonesha hali hiyo.

Polisemia


leksimu	chui	mnyama anayekula nyama anafanana na paka
		→
fahiwa	ukali	mtu mwenye ukali mwingi hasa wenye kudhalilisha
		→
Wakati		→

Kutokana na mchoro huu inabainika kwamba sitari ni mbinu ya kupanua maana ya neno katika lugha inayozingatia mfanano kati ya dhana zinazohusika. Katika sitari “Ali ni fisi” tunaelewa kuwa fisi (Mnyama) anayo sifa ya ulafi. Kwa hivyo ili Ali aweze kuwa fisi ni lazima pia awe na sifa za ulafi kama fisi. Kwa hivyo ni hali hii ambayo inapelekea kulinganisha fisi na Ali. Hapa, eneo chasili ni Ali na fisi. Kwa upande mwingine, eneo lengwa ni ulafi. Mchakato utakuwa:



Matumizi ya leksimu ‘fisi’ yamepelekea leksimu hiyo kuwa na maana ya ziada ili kuunda polisemi. Kwa sasa leksimu ‘fisi’ ina maana mbili ambazo ni: 1. mnyama wa mwituni mwenye ukubwa kama beberu, aliye na rangi ya kijivu na anayeaminiwa kuwa ni mwoga na anayependa sana kula mizoga. 2. Mtu mlafi.


Katika sitiari “Riziki ni kupe”, hapa Riziki amefungwa kwenye ‘kupe’ na kweli tunafahamu kuwa kupe ni mdudu ambaye hutegemea wanyama wengine kwa manufaa ya kibinafsi. Kwa hivyo ili Riziki awe kupe ni lazima pia awe na sifa ya utegemezi kama vile ya kupe. Ni kupitia katika utaratibu huu ndiposa tunapata maana ya ziada ya kupe. Hali hii inaweza kuwasilishwa kimchoro kama ifuatavyo:



Mchoro wa hapo juu unaonyesha kuwa katika eneo chanzo, Riziki anahusishwa na kupe lakini kisitiari anayo sifa ya utegemezi. Ni katika utaratibu huu

ambapo dhana ‘kupe’ inapata maana ya pili; Mtu anayepata mapato bila kutumia jasho lake.

Kuna baadhi ya leksimu ambazo zina maana zaidi ya mbili katika *Kamusu ya Kiswahili Sanifu 2018*. Kwa mfano, ‘jicho’ unapochunguza maana za ziada za leksimu hiyo, utabaini kuwa zimepanuka kiistiari na kuzalisha maana mpya kutoka kwa ya kwanza. Kwa hivyo matumizi haya ya ziada ya leksimu ‘jicho’ yanapoendelea kutumika katika miktadha mbalimbali yanaunda polisemi ambapo leksimu ‘jicho’ kwa sasa ina maana zifuatazo: (i) kiungo cha mwili cha kuonea. (ii) panda liwekwalo katika gubeti ya jahazi. (iii) chipukizi la ua. Hali hiyo inaweza kuonyeshwa kimchoro ifuatavyo:




Mchoro 4.4: Leksimu ambazo zina maana zaidi ya mbili

Kielezo cha hapo juu kinaonyesha kuwa katika kiwango cha chanzo, leksimu ‘jicho’ imepanuka kisitiari na kupata maana za ziada. Pia imebainika kuwa maana za leksimu ‘jicho’ huunganishwa pamoja kupitia utaratibu wa

kisemantiki wa kawaida (umbo la mpangilio au taswira) ambayo inawakilisha seti ya sifa za kidhahania zinazoshirikishwa. Hali hii inashabihiana na mhimili wa semantiki tambuzi unaodai kwamba binadamu ana umilisi mkubwa wa kiutambuzi wa kuhamisha dhana kutoka wanda moja la maarifa hadi jingine. Hali hii huchangia upanuzi wa maana ya leksimu zinazohusika. Kwa mfano, kutokana na muktadha wa matumizi ya leksimu ‘jicho’ maana lengwa hubainika wazi.

Maana za leksimu ‘beberu’ katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)* zimeorodheshwa zikiwa tano; (i) mbuzi dume (ii) mwanamume mwenye nguvu (iii) mtu anayetoa harufu mbaya (iv) taifa linalotawala nchi nyingine kiuchumi au kisiasa (v) mtu anayeamini na kutekeleza siasa ya ubeberu. Tukichunguza maana ya awali ya leksimu ‘beberu’ (mbuzi dume) tutabaini kuwa maana hiyo imepanuka na kuhusisha dhana za kandokando. Hali hiyo inaweza kuwasilishwa kimchoro ifuatavyo:



Mchoro 4.5: Upanuzi wa Istiari


Mchoro huu wa hapo juu unaonesha kuwa leksimu ‘beberu’ imepanuka kisitiari na kuzua maana zingine ambazo zina uhusiano na maana msingi ya leksimu hiyo. Wanasemantiki tambuzi hueleza kuwa maana hujumuisha maana awali pamoja na fahiwa zake zote. Kwa hivyo, aliye na umilisi wa leksimu ‘beberu’ pia hufahamu sifa zake kama vile usumbufu, familia yake na tabia yake ya kujikojolea. Kwa mfano, kauli; Yule (X) ni beberu. Binadamu ambaye ana umilisi wa lugha atabaini kuwa anayerejelewa (X) ni binadamu na wala si mnyama.

4.2 Mchakato ambao metonimu hupitia kuunda polisemi

Kama ilivyoelezwa katika sura zilizotangulia, dhana ya metonimu imejadiliwa na wataalamu mbalimbali, baadhi ya hao ni Chacha na Pendo (2019) ambao wanafasili metonimu kuwa ni tamathali ya usemi inayotumiwa katika lugha ambapo kitu au dhana haitajwi kwa jina lake ila kwa jina la kitu au dhana nyingine inayohusiana nayo kwa karibu. Kwa mfano, ‘Westminister’ ni metonimu ya Bunge la Uingereza. Kwa upande mwingine, Mbatiah (2001)

anaeleza kuwa japo fahiwa ya metonimu huangaziwa katika semantiki, fahiwa hii pia hutumiwa na wanafasihi ambapo fasili yake hutokana na kutajwa kwa sifa ya kitu ili kudokeza maana kusudiwa badala ya kitu chenyewe. Kwa hivyo kutokana na maelezo hayo, metonimu ni mchakato ambapo neno au jina linatumiwa kurejelea kitu kingine ambacho kinahusiana na hicho cha kwanza kwa namna fulani.


Kama ilivyo katika sitiari, pia metonimu za kimawazo hutumiwa kuunda polisemia. Tofauti na sitiari, metonimu huwa na eneo moja la kimawazo. Ufahamu wa binadamu umegawanywa katika maeneo. Metonimu ni ubadilishaji wa jina kati ya vitu viwili ambavyo vinahusiana kwa karibu. Katika metonimu, kitu kimoja kinasimamia kingine katika eneo moja. Kwa mfano, virejelewa kiti (R_i) na uongozi (R_j) viko katika eneo moja, na kwa hivyo vipo katika uhusiano au ujirani wa karibu. Kwa hiyo, katika metonimu kitaja ndicho kinachobadilika lakini kitajwa hubakia kile kile. Angalia mchoro huu.



Maana zinazopatikana hutokana na upanuzi wa maana kimetoni kuunda polisemi. Katika metonimu, jina hilo jingine lililotumiwa kwa maana ya kirejelewa cha awali ndilo hupata maana ya ziada. Kwa mfano, hapo juu neno


'kiti' linakuwa na maana zaidi ya moja: 1. kifaa kilichotengenezwa kwa madhumuni ya kukalia 2. nafasi ya uongozi.

Metonimu 'dishi' pia imepitia mchakato ili kuunda polisemi. Kabla ya dhana hii kupanuka kimetonimu ilikuwa ikirejelea sahani kubwa ya kupakulia chakula. Kutokana na upanuzi wa maana kimetonimu kuunda polisemi, dhana 'dishi' ilipanuka na kuwakilisha eneo la chakula ndiposa tunapata dhana kama vile 'dishi ya wali'. Ifahamike kwamba metonimu hutokea tu kati ya maneno ambayo tayari yana uhusiano. Hali hiyo inaweza kuwakilishwa kimchoro ifuatavyo:




Mchoro 4.5: Metonimu

Kielelezo hiki cha pambetatu kinaonyesha kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya eneo na leksimu, na kitajwa na leksimu. Kwa hivyo, leksimu 'dishi' imepata maana ya ziada na kurejelea chakula kilichomo kwenye dishi. Uhusiano unaojitokeza hapa ni ule wa chombo kwa kitu kilichomo kwenye chombo hicho. Tazama mchoro huu:



Lakoff na Mark (1989) wanaeleza kuwa asili ya lugha ya kimetonimu hutokana na maneno kusimamia dhana zinazozielezea kwa kuwa hakuna njia nyingine ya kueleza na kuwasilisha dhana isipokuwa kwa kutumia maumbo ya lugha pamoja na mifumo mingine ya mawasiliano. Kile ambacho wataalamu hao wanamaanisha ni kuwa katika metonimu, neno lina uwezo wa kusimamia dhana fulani katika lugha ya Kiswahili. Tazama mchoro ulio hapo chini:



Hapa tunaona kuwa neno ‘familia’ limewakilisha eneo ambalo ni jengo. Hii ni kutokana na hali ya neno hilo kupanuka kimetonimu na kupata maana mpya ya ziada ili kuunda polisemi. 1. jengo ambalo limekusudiwa kukaliwa na watu. 2. familia.

4.3 Hitimisho

Lengo la sura hii lilikuwa ni kuchunguza mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia ili kuunda polisemi katika Kiswahili. Sura hii ilionyesha kwamba sitiari hupitia utaratibu fulani ili kuzua polisemi. Utaratibu huo hutokana na uhusiano uliopo katika maeneo ya sitiari ambayo ni eneo chasili na eneo lengwa. Pia tulibainisha kuwa metonimu huwa na eneo moja ambalo huwa na uhusiano wa ujirani. Vilevile sura hii ilibaini kuwa mchakato wa sitiari na metonimu hutokana na upanuzi wa leksimu ili kuunda polisemia katika lugha ya Kiswahili.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

5.0 Utangulizi

Katika Sura ya Nne, mtafiti ameonyesha mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia kuunda polisemia katika Kiswahili. Imebainika kuwa sitiari na metonimu hupitia katika utaratibu fulani ndiposa zikazalisha maana ya pili kutoka kwa ya kwanza. Katika sura hii, mtafiti ametoa muhtasari wa sura mbalimbali za utafiti huu, matokeo na kutoa mapendekezo ya tafiti zingine zaidi ambazo zinaweza kutekelezwa baadaye kuhusu namna ambavyo mbinu zingine za lugha zinaweza kuchangia katika taaluma ya semantiki na lugha kwa jumla.

5.1 Muhtasari wa tasnifu

Katika Sura ya Kwanza, mtafiti ameonyesha usuli wa mada ambapo aliweka bayana eneo ambalo mada ya utafiti inapatikana. Mtafiti amebainisha suala la utafiti ambapo alifafanua kuwa unapochunguza matumizi yaliyokolea ya sitiari na metonimu bado si wazi mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia ili kuunda dhana ya pili kutoka kwa ya kwanza. Pia, mtafiti amebainisha malengo ya utafiti ambayo yalimwongoza mtafiti katika kufanya utafiti huu.

Malengo ya utafiti huu ni: kubainisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu katika Kiswahili, kuainisha polisemi katika lugha ya Kiswahili na kudhihirisha mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia kuunda polisemi katika Kiswahili. Pia, mtafiti alionyesha nadharia ambayo iliongoza mchakato mzima wa utafiti huu. Nadharia yenyewe ni nadharia ya semantiki

tambuzi ambayo baadhi ya waitifaki wake ni: Lakoff (1987), Langacker (1987) na Lemmens (2017) na kubainisha mihimili yake. Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo katika kuwasilisha matokeo. Uchunguzi huu umefanyika maktabani ambapo majarida, tasnifu na makala ya mtandaoni pia yametumika. Data iliyochanganuliwa katika utafiti imedondolewa kutoka kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2018) kwa kuongozwa na mbinu ya usomaji na udondoaji ambapo mtafiti aliweza kudondoa polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu.

Katika Sura ya Pili, mtafiti amechunguza lengo la kwanza ambalo ni kubainisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu. Mtafiti ameanza kwa kubainisha polisemi kutoka kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2018) ambazo zimeundwa kutokana na sitiari. Baadaye mtafiti amebainisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na metonimu. Katika sehemu hii polisemi hamsini na sita zinazoundwa kutoka na sitiari na metonimu zilibainishwa.

Katika Sura ya Tatu, mtafiti ameanisha polisemi katika makundi mbalimbali. Katika kuziainisha polisemi hizo, mtafiti ametumia vigezo kama vile kigezo cha kiutambuzi. Uainishaji huu umehusisha polisemi za viumbe hai. Kwa mfano, wanyama na binadamu. Uainishaji wa kiuamilifu nao umehusisha polisemi za utendakazi. Uainishaji wa kijiografia nao umehusisha polisemi za mahali kama vile makao. Uainishaji wa polisemi kwa mtazamo wa kitabia pia umehusisha polisemi za viumbe hai. Data katika Sura ya Tatu imechanganuliwa na kuwasilisha matokeo kwa njia ya majedwali.

Katika Sura ya Nne, mtafiti ameonyesha mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia kuunda polisemi katika Kiswahili. Mtafiti ametanguliza kuonyesha mchakato ambao sitiari hupitia kuunda polisemi kisha baadaye ameonyesha mchakato ambao metonimu hupitia kuunda polisemi. Data katika Sura ya Nne, imechanganuliwa na kuwasilisha matokeo kwa njia ya maelezo na michoro.

5.2 Matokeo ya utafiti

Mtafiti aliwasilisha matokeo ya utafiti huu kwa njia ya majedwali, michoro na maelezo kulingana na malengo matatu ya utafiti. Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu katika Kiswahili. Utafiti huu ulijikita maktabani ambapo mtafiti aliweza kudondoa polisemi hamsini na sita ambazo zimeundwa kutokana na sitiari na metonimu kutoka kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2018). Katika Sura ya Pili, imedhihirika kuwa kuna baadhi ya polisemi zilizojitokeza ndani ya homonimu kwa mfano, *tata*² na *chuo*¹. Pia imebainika kuwa idadi kubwa ya sitiari imechangia katika kuunda polisemi ikilinganishwa na metonimu. Kwa mfano, sitiari arobaini na metonimu kumi na tano zilidondolewa kutoka kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2018). Baadhi ya sitiari na metonimu zilizodondolewa ni: *chui, ndumakuwili, chiriku, fisi, jicho, kasuku, kupe, kiti, dishi, fedha na ikulu*.

Lengo la tatu lilikuwa kuainisha polisemi katika lugha ya Kiswahili. Katika sura ya tatu, mtafiti aligawa polisemi katika makundi mbalimbali kwa misingi ya vigezo. Kwa mfano, uainishaji wa kiutambuzi. Uainishaji hurejelea vitu kwa mujibu wa jinsi vitu hivyo vinavyofanana na vinavyoonekana. Katika

uainishaji huu, polisemi za sehemu za mwili zilibainishwa. Kwa mfano, *mguu* na *mkono*. Pia kuna kigezo cha uainishaji wa polisemi kwa mtazamo wa kitabia. Uainishaji huu nao ulijikita katika viumbe hai. Katika kumbo hili, utafiti ulibainisha aina tatu za polisemi zifuatazo: polisemi za wadudu, polisemi za wanyama na polisemi za ndege.

Vilevile, kuna kigezo cha uainishaji wa kiuamilifu. Uainishaji huu ulirejelea kazi zinazofanywa na vitu fulani maalumu katika uwanda wa kileksika. Katika kumbo hili, aina mbili za polisemi zilibainishwa: polisemi za utendakazi wa kitu na polisemi za chombojikoni. Imebainika kuwa baadhi ya polisemi ziliweza kugawika katika zaidi ya kundi moja. Kwa mfano, katika uainishaji wa polisemi za kiutambuzi, leksimu ‘mkono’ na ‘mguu’ ziliainishwa kama polisemi za sehemu za mwili.

Pia, leksimu hizo ziliainishwa katika kumbo la kiuamilifu kama polisemi zinazorejelea utendakazi wa kitu. Pia, imebainika kuwa polisemi zimepanuka kisitiari kumaanisha dhana nyingine katika muktadha tofauti. Kwa mfano, Katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018)*, neno *Jicho* maana zake zimeorodheshwa zikiwa tatu; (i) kiungo cha mwili cha kuonea. (ii) panda liwekwalo katika gubeti ya jahazi. (iii) chipukizi la ua. Kwa hivyo, maana ya msingi leksimu ‘jicho’ imepanuka kisitiari na kuwasilisha dhana nyingine kama vile, jicho la viazi, jicho la sindano na jicho la mihogo.

Lengo la tatu lilikuwa kudhihirisha mchakato ambao sitiari na metonimu hupitia kuunda polisemi katika Kiswahili. Imebainika kuwa sitiari huwa na maeneo mawili ya ufahamu: moja ni ile inayotokana na maumbo tunayoyaona

na nyingine ni ile ya kidhahania. Hiyo ya kwanza inaitwa eneo chasili/chanzo na ya pili inaitwa eneo lengwa. Kwa mfano, sitiari ‘Maria ni chui nyumbani’ kumaanisha Maria ni mkali akiwa nyumbani. Eneo chasili katika sitiari hiyo ni Maria na chui. Kwa upande mwingine, eneo lengwa ni sifa ya ukali ya chui. Kwa hivyo, dhana mpya hutokana na kulinganisha maeneo haya mawili ya sitiari.

Pia, imebainika kuwa sitiari huwa na sehemu tatu: kifananishi, kiungo na kizungumzwa ambazo zinachangia katika uzuaji wa polisemi katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, katika sitiari *Maria ni chui nyumbani*, kifananishi ni chui, kizungumzwa ni Maria na kiungo ni ukali. Kwa upande mwingine, imebainika kuwa metonimu huwa na eneo moja. Kwa mfano, leksimu *kiti* eneo lake ni uongozi. Vilevile kulingana na data ya utafiti huu, polisemi ambazo zimeundwa kutokana na metonimu ni chache mno ikilinganishwa na polisemi ambazo zimeundwa kutokana na sitiari.

5.3 Mapendekezo ya utafiti

Kutokana na matokeo ya uchunguzi huu, mtafiti ameweza kutoa mapendekezo ya utafiti yafuatayo: Kwanza, kuna haja ya tafiti zingine kufanywa kuhusu mchango wa mbinu zingine za lugha kama vile tashibihi na jazanda yaani namna ambavyo mbinu hizo zinaweza kuchangia pia katika kuunda polisemi katika Kiswahili. Pili, kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu dhana ya polisemi kwa kuzingatia kamusi na nadharia nyinginezo ili kuongeza maarifa zaidi katika lugha. Tatu, mtafiti amekumbana na tafiti chache zilizoshughulikia

mchango wa sitiari na metonimu katika kuunda polisemia katika Kiswahili.

Hivyo basi, kuna haja ya kuwa na tafiti zaidi zinazolenga sehemu hii.

5.4 Hitimisho

Utafiti huu umeshughulikia mchango wa sitiari na metonimu katika kuunda polisemia katika Kiswahili. Imebainika kuwa mbinu za sitiari na metonimu zina mchango mkubwa katika kuunda polisemi. Pia sura hii imetoa muhtasari wa yale mtafiti ameshughulikia katika kila sura ya utafiti huu. Pia imeweza kueleza matokeo ya utafiti huu kulingana na malengo ya utafiti. Vilevile, mapendekezo ya utafiti huu yaliweza kubainishwa ambapo mtafiti ameeleza tafiti zingine zinazoweza kufanywa ili kuzalisha maarifa zaidi.

MAREJELEO

- Berg, L.K. (2001). *Qualitative Research Methods for the Social Sciences*. California: Pearson Education Company.
- Bynon, T. (1977). *Historical Linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Chacha, L.M. & Pendo, S.M. (2019). *Semantiki*. Nairobi: Longhorn Publishers
- Creswell, J.W. (2007) *Educational Research Planning and Evaluation: Qualitative and Quantitative Research* (2ed). Ohio: Prentice Hall, Inc.
- Creswell, W. J. (2014). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed-method approaches* (4th ed.). Thousand Oaks, CA: Sage.
- Edwin, O. M. (2015). *Vitendo Sogezi katika Kiswahili Sanifu*. Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa), katika Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Evans, V. & Green, M. (2006). *Cognitive Linguistic: An Introduction*. Endinburgh University Press.
- Gaichu, N. M. (2016). *Uchunguzi wa Sitiari Dhanifu katika Methali za Kiswahili Mtazamo wa Nadharia ya uhusiano*. Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Gardenfors, P. (1999). Some Tenets of Cognitive Semantics. Katika Allwood, J. & Gardenfors, P. (Wah) *Cognitive Semantics: Meaning and cognition* (Uk. 19-30) Amsterdam. John Benjamin Publishing Company.
- Gichuru, T. M. (2020). *Mabadiliko ya Maana za leksia za Kiswahili: mtazamo linganishi wa kikale na kisasa*. Tasnifu ya uzamifu (Haijachapishwa) Katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Kibiki, M. J. & Malangwa, P. (2012). *Mabadiliko ya Maana katika Vitenzi vya Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri katika Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kitundu, G. J. & Malangwa, P.S. (2020). Ujenzi wa Maana katika Sitiari na Tashibiha za Kiswahili. *Kioo cha lugha, 17(1)*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Lakoff, G & Mark T. (1989). *More than cool Reason: A Field Guide to Poetic Metaphor*. Chicago University Press.
- Lakoff, G. (1987). *Women, Fire and Dangerous Things*. Chicago: University of Chicago Press

- Langacker, R.W. (1987). *Foundation of Cognitive grammar: Theoretical Perspectives*: Stanford: Stanford University Press.
- Lemmens, M. (2017). 'Cognitive Semantics' in *Routledge Handbook of Semantics*. Editor Nick Riemer. London and New York: Routledge.
- Makame, H.O. (2015). *Maana za Kisitari Zinavyojitokeza katika Nomino za Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri katika Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mapunda, G. na Ngunguti, M. (2021). *Tafakuri ya Upolisemia na Usitari wa Ungonoshaji wa Maneno katika Kiswahili cha Mazungumzo*. Retrieved from <https://www.researchgate.net/publication/355788980>.
- Marshall, C. & Rossman, B.G. (1995). *Designing Qualitative Research*. London: SAGE Press.
- Masharipova, N. (2020). The Functional Features of Polysemy in English and Uzbek Languages. *International Journal of Innovative Technologies in Social Science*. 2(23).
- Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Textbook Graphic Publishing.
- McCasland, S.V. (1949). Some New Testament Metonyms for God. *Journal of Biblical Literature*, Jun., 1949, Vol. 68, No. 2 (Jun.,1949), pp. 99-113 P: The Society of Biblical Literature Stable Retrieved from URL: <https://www.jstor.org/stable/3261996>.
- Mdee, J. S., Njogu. K., & Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn.
- Milroy, A.L. (1987). *Observing and Analysing Natural Languages*. Oxford: Basil Blackwell.
- Mugenda, O. M & Mugenda, A.G. (1999). *Research Methods. Quantitative Approaches and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.
- Mugenda, O.M & Mugenda, A.G. (2019). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: ACTS Press.
- Mugenda, O.M. & Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: ACTS Press.
- Mulokozi, M. na Kahigi, K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

- Mwendamseke, F. J. (2016). Uelekeo wa Maana za Kipolisemia katika Msamiati wa Kiswahili: Mifano kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Kioo cha Lugha, 14* (39-49). Dar es Salaam: TUKI.
- Ndirangu, D.M. (2011). “*Kenyan Indegenous Redio Stations and their uses of Metaphor in 2007 Election Violence*”. https://www.researchgate.net/publication/272206134_Kenya's_indigenous_radio_stations_and_their_use_of_metaphors_in_the_2007_election_violence.
- Okal, O. B. (2018). *Uchunguzi wa Kileksikografia wa Hiponimia za Leksimu Nomino na vitenzi Vya Kiswahili na Tafsiiri zake katika Kuluo. Tasnifu ya uzamifu katika Kiswahili* (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Maseno.
- Rajab, T. W. (2017). *Mabadiliko ya Maana ya Msamiati wa Kiswahili katika Mkutadha wa Kisiasa: mfano kutoka katika hotuba za kampeni uchaguzi 2015. Tasnifu ya uzamili katika Kiswahili* (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Sun, B. (2019). Cognitive Interpretation of polysemy, Retrieved from, https://www.researchgate.net/publication/338246639_Cognitive_Interpretation_of_Polysemy/link/5e0ab224a6fdcc28374adfec/download.
- TUKI, (2018). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Ullmann, S. (1967). *Semantics: An introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell.
- Vyvyan, E. & Greens, M. (2006). *Cognitive Linguistics. An Introduction*. Edinburgh: Edinburgh University Press.
- Zoltán, K. (2013). The Metaphor–Metonymy Relationship: Correlation Metaphors Are Based on Metonymy, *Metaphor and Symbol*, Retrieved from 28:2, 75-88, DOI: 10.1080/10926488.2013.

VIAMBATISHO

Kiambatisho A: Kibali cha kukubalika kwa pendekezo



KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Website: www.ku.ac.ke

Internal Memo

FROM: Dean, Graduate School

DATE: 17th August, 2022

TO: Mark Elphas Masika
C/o Kiswahili & African Languages Dept.

REF: C50/28186/2019

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROJECT PROPOSAL

This is to inform you that Graduate School Board at its meeting of 17th August, 2022 approved your Research Project Proposal for the M.A Degree Entitled, "Mchango wa Sitiari na Metonimu Katika Uzuaji wa Polisemia Katika Kiswahili."

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed supervision tracking and progress report forms per semester. The forms are available at the university's website under Graduate School webpage downloads.

Also, please ensure that you publish article(s) from your project before submitting it to Graduate School for examination as per the Commission for University Education and Kenyatta University guidelines.

Thank you.

ELIJAH MUTUA
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

c.c. Chairman, Kiswahili and African Languages Department

Supervisors:

1. Dr. Leonard Mwita Chacha
C/o Department of Kiswahili & African Languages
Kenyatta University

EM/mo

Kiambatisho B: Kibali cha idhini ya kutekeleza Utafiti**KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL**E-mail: dean-graduate@ku.ac.keP.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530Website: www.ku.ac.ke

Our Ref: C50/28186/2019

DATE: 17th August, 2022Director General,
National Commission for Science, Technology
and Innovation
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI

Dear Sir/Madam,

RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR MARK ELPHAS MASIKA - REG. NO. C50/28186/2019

I write to introduce Mark Elphas Masika who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the Department of Kiswahili & African Languages.

Mark intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, "Mchango wa Sitiari na Metonimu Katika Uzuaji wa Polisemia Katika Kiswahili."

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours, faithfully,

A handwritten signature in blue ink, appearing to be 'E. Kimani'.

/ **PROF. ELISHIBA KIMANI**
DEAN, GRADUATE SCHOOL

EM/mo

Kiambatisho C: Kibali cha NACOSTI



NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Date of Issue: **04/October/2022**

Ref No: **968406**

RESEARCH LICENSE



This is to Certify that **Mr. Mark Elphas Masika** of **Kenyatta University**, has been licensed to conduct research in **Nairobi** on the topic: **MCHANGO WA SITIHARINA METONIMU KATIKA UZUAJI WA POLESEMIA KATIKA KISWAHILI** for the period ending: **04/October/2023**.

License No: **NACOSTI/P/22/20698**

Applicant Identification Number: **968406**


 Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code



NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013

The Grant of Research Licenses is Guided by the Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

CONDITIONS

1. The License is valid for the proposed research, location and specified period
2. The License any rights thereunder are non-transferable
3. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research
4. Excavation, filming and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies
5. The License does not give authority to transfer research materials
6. NACOSTI may monitor and evaluate the licensed research project
7. The Licensee shall submit one hard copy and upload a soft copy of their final report (thesis) within one year of completion of the research
8. NACOSTI reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice

National Commission for Science, Technology and Innovation
 off Waiyaki Way, Upper Kabete,
 P. O. Box 30623, 00100 Nairobi, KENYA
 Land line: 020 4007000, 020 2241349, 020 3310571, 020 8001077
 Mobile: 0713 788 787 / 0735 404 245
 E-mail: dg@nacosti.go.ke / registry@nacosti.go.ke
 Website: www.nacosti.go.ke